

UTAYARI SHAJI  
WA  
MPANGO KABAMBE WA TAI FA WA UMWAGILIAJI  
KATIKA  
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Rasimu ya Mwongozo

wa

Uandaaji wa Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji  
Maji Mashambani Ndani ya Mpango wa  
Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya



Desemba 2004

NIPPON KOEI CO., LTD.  
NIPPON GIKEN INC.

RD

JR

04-32

SHIRIKA LA MAENDELEO YA KIMATAIFA LA JAPANI (JICA)  
WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA (WKC)

UTAYARISHAJI  
WA  
MPANGO KABAMBE WA TAIFA WA UMWAGILIAJI  
KATIKA  
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# **Rasimu ya Mwongozo**

wa

**Uandaaji wa Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji  
Maji Mashambani Ndani ya Mpango wa  
Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya**

Desemba 2004

NIPPON KOEI CO., LTD.  
NIPPON GIKEN INC.

Kwa yeyote atakayehusika

Nakala hii ya Kiswahili imetafsiriwa kutoka ile ya Kiingereza ya Rasimu ya Mwongozo wa Uandaaji wa Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mshambani Ndani ya Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Hii ni kwa ajili ya kurejea (reference) tu. Kwa matumizi ya ofisi, unashauriwa kutumia nakala ya Kingereza.

## Matumizi ya Mwongozo

### **1. Kitu gani kimeelezwa katika mwongozo?**

Mwongozo huu unaelekeza njia ya haraka na ya vitendo katika kuandaa skimu za umwagiliaji chini ya Mpango wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji katika Wilaya (DADPs). Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba, watumishi wa wilaya ni lazima wafuate taratibu au viwango vilivyopo katika mwongozo huu. Mwongozo huu unalenga kutumika katika uandaaji wa skimu za umwagiliaji zinazo endeshwa na wakulima wadogo katika wilaya (inahusisha skimu za umwagiliaji kwa njia ya mteremko, kwa njia ya kutumia pampu ambazo chanzo kikuu cha maji ni mto au dimbwi au ziwa pamoja na uvunaji wa maji) kwa kutilia maanani mafungu ya fedha yaliyopo katika DADP pamoja na uzoefu wa watumishi wa wilaya.

### **2. Kwa nini Mwongozo huu umetayarishwa?**

Mwongozo huu ulitayarishwa mwaka 2003 ikiwa moja ya shughuli muhimu za Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) ambayo ilikamilika November 2002. Chini ya programu hii Wilaya nyingi zilibunika skimu za umwagiliaji. Hata hivyo, iligundulika kwamba miradi mingi iliyobuniwa ilishindwa kukidhi matarajio yaliokusudiwa katika mipango ya maendeleo. Kwa kutambua mapungufu haya, iliamuliwa kutayarisha Mwongozo wa Uandaaji wa Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani kwa Ajili ya Mpango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs).

### **3. Mwongozo huu umetayarishwa kwa ajili ya nani?**

Mwongozo huu umetayarishwa mahususi kwa ajili ya watumishi wa wilaya wanaojihusisha na sekta ya kilimo ambao wanaohusika katika maandalizi ya Mipango ya Kuendeleza Kilimo ya Wilaya (DADP). Vile vile mwongozo huu ni muhimu kwa watumishi waliopo katika ofisi za umwagiliaji za kanda kwa kuwa wana nafasi muhimu katika kushiriki uandaaji wa Mipango ya Kilimo ya wilaya kama vile kuthibitisha mipango ya wilaya pamoja na usimamiaji wake kiufundi.

### **4. Mwongozo huu umetayarishwaje?**

Mbinu shirikishi ilitumika katika kuandaa mwongozo huu kwa kutumia majaribio yaliyo fanywa katika wilaya ambapo mwongozo uliboreshwa pale ilipobidi na wataalam kutoka wilayani, ofisi ya umwagiliaji kanda na watumishi wa Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi.

### **5. Mwongozo huu una sifa gani muhimu?**

Matumizi ya mwongozo huu ni wa haraka na wa vitendo katika kuandaa mipango ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika DADP.

## Matumizi ya Maneno

Katika mwongozo huu, maneno yafuatayo yamefafanuliwa katika jedwali hapa chini. Hata hivyo, haimaanishi kwamba muda wote yanapotumika lazima yawe na maana ileile kama ilivyo fafanuliwa, kwa mfano yanapotumika nje ya mwongozo huu. Neno fulani linaweza kutumiwa kwa maana tofauti na iliyo elezewa katika mwongozo huu.

<b>1. Timu na kamati</b>	
<i>Timu ya wilaya ya kuendeleza mradi (DPDT)</i>	I taundwa timu moja kwa kila wilaya kwa ajili ya kuandaa mipango ya skimu za umwagiliaji kwa ajili ya DADP. Timu hii itaundwa na wataalam wafuatao, Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya kama mwenyekiti (DALDO), Mtaalamu wa umwagiliaji wa wilaya (SMS), Mtalaamu wa kilimo wa wilaya (SMS), Afisa ugani na watumishi wengine muhimu wa ofisi ya wilaya, viongozi wawakilishi toka tarafani, Viongozi katika vijiji, Wawakilishi wa wakulima, na baadhi ya wadau wengine kama itakvyopendekezwa na Halmashauri ya Wilaya pamoja na vyama visivyo vya kiserikali kama itakuwa muhimu.
<i>Kamati ya mapitio ya kanda (ZRC)</i>	Kamati itaundwa katika kila kanda ya umwagiliaji (ZIU), kwa ajili ya kutathmini na kuidhinisha mapendekezo ya uundaji wa miradi ya umwagiliaji kwa ajili ya DADP kama itakavyotayarishwa na DPDT. Timu hii itakuwa na Afisa Kanda kama mwenyekiti, wataalamu wa aina mbali mbali katika fani ya umwagiliaji, kilimo, udongo na mazingira.

<b>2. Upimaji wa eneo na Upangaji</b>	
<i>Ukaguzi wa haraka katika eneo</i>	Upimaji wa maeneo yote ya skimu katika wilaya ufanyike, ili kuchagua maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji kwa ajili ya kutayarisha mipango ya awali.
<i>Upimaji wa eneo (Field Survey)</i>	Zooezi hili lifanyike kwa skimu zilizo chaguliwa kwa njia ya uchujaji (screening).
<i>Mpango wa awali</i>	Mipango kwa ajili ya skimu za umwagiliaji zilizo chaguliwa kwa njia ya uchujaji (screening).

<b>3. Kutoa Taarifa na Nyaraka</b>	
<i>Taarifa ya ukaguzi wa eneo pamoja na uchambuzi</i>	Taarifa hii iandaliwe na DPDT ikielezea matokeo ya uchambuzi. Taarifa iwasilishe kwa ZRC kwa ajili ya tathmini na kuidhinisha.
<i>Barua ya kuidhinisha uchambuzi</i>	Barua iandaliwe na ZRC ili kuidhinisha matokeo ya uchambuzi yaliyofanywa na wilaya.
<i>Barua ya kuthibisho eneo lililopendekezwa</i>	Barua itayarishwe na serikali ya kijiji kuthibitisha kuwa wanakijiji wamekubali kuhusu eneo lililopendekezwa (eneo ambalo litaingia katika mpango wa awali).
<i>Taarifa juu ya mipango ya kuandaa skimu za umwagiliaji</i>	Taarifa itayarishwe na DPDT na kuambatanisha matokeo yote ya upimaji wa eneo, mipango ya mwanzo, kipaumbele cha skimu pamoja na programu za wilaya. Takwimu zote zijazwe kwenye fomu na ziambatanishwe ramani zilizotayarishwa kulingana na skimu zilizoteuliwa.
<i>Barua ya kuhalalisha na makubaliano</i>	Barua zitatarishwa na ZRC ili kuhalalisha na kukubaliana juu ya matokeo ya mipango ya maendeleo ya umwagiliaji iliyofanywa na wilaya.

4. Ramani	
<i>Ramani ya maliasili ya kijiji</i>	Ramani iliyotayarishwe na wanakijiji kuonyesha rasilimali zilipo kama vile mito, ardhi ya kilimo n.k.
<i>Ramani inayoonyesha hali ya sasa</i>	Ramani iliyotayarishwa na DPDT ikionyesha mali asili za kijiji mahali zilipo kwa usahihi zaidi kwa kutumia kifaa cha GPS. Vipimo vya kodineta vionyeshwe katika karatasi husika.
<i>Ramani inayoonyesha mpango wa kuendeleza skimu</i>	Ramani iliyotayarishwa na DPDT ikionyesha hali ya sasa ambayo mbali na kuonyesha mali asili zilizopo, vile vile inaonyesha sehemu zitakazo jengwa banio, mifereji, barabara n.k.

5. Eneo	
<i>Eneo linalofaa kuendelezwa,</i>	Eneo linalofaa kuendelezwa na wanakijiji katika Fursa na Vikwazo katika Maendeleo (mpango wa kijiji)
<i>Eneo linalolimwa</i>	Eneo linalolimwa kati ya eneo linalofaa kuendelezwa
<i>Eneo linalomwagiliwa</i>	Eneo linalomwagiliwa hivi sasa
<i>Eneo linalotegemea mvua</i>	Eneo ambalo linalimwa kwa kutegemea mvua
<i>Eneo linalopendekezwa</i>	Eneo linalofikiriwa kuingizwa katika mpango wa awali. Maeneo yachaguliwe na wanakijiji kama ni kipaumbele chao katika mkutano wa upimaji. Wanakijiji watatakiwa kuthibitisha katika kikao baada ya kufanya ukaguzi wa eneo kwa kuandika barua na kuituma kwa ofisi ya wilaya kutoka serikali ya kijiji.
<i>Eneo linalo mwagiliwa wakati wa masika</i>	Eneo linalo mwagiliwa wakati wa masika
<i>Eneo linalo mwagiliwa wakati wa kiangazi</i>	Eneo linalo mwagiliwa wakati wa kiangazi
<i>Eneo linalo endekezwa</i>	Eneo litakalo endekezwa (eneo litakalo jengewa miundo mbinu tya umwagiliaji)
<i>Eneo linaloweza kumwagiliwa</i>	Eneo ambalo linaweza kumwagiliwa kwa ujumla wake. Hii ni sawa na eneo litakalo endekezwa, isipokuwa kama eneo lililopendekezwa ni upanuzi wa mfereji uliopo. Kwa skimu ambayo inapanuliwa, eneo litakalomwagiliwa litajumuisha eneo lililopo pamoja na eneo la ziada ambalo litakalo endekezwa.

6. Mfumo wa Umwagiliaji	
<i>Skimu ya umwagiliaji</i>	Skimu ya Umwagiliaji inatakiwa kukidhi matakwa yafuatayo ili iweze kutambulika kama skimu. <ol style="list-style-type: none"> <li>1) I we na mifereji inayochukua maji kutoka katika banio.</li> <li>2) I we na mabanio yaliunganishwa na mifereji kwa ajili ya umwagiliaji.</li> <li>3) I we na mabanio pamoja na mifereji iliyo sambaa lakini banio na mfereji mkuu uwepo katika kijiji kimoja.</li> </ol>
<i>Skimu ya umwagiliaji wa jadi</i>	Skimu ilioanzishwa na kuendeshwa na wakulima wenyewe bila kusaidiwa na watu au mashirika kutoka nje. Hii inajumuisha mifereji ya umwagiliaji maji ya jadi kwa ajili ya kuzalisha matunda na mbogamboga kutoka nyanda za juu pamoja na skimu zinazo tumia njia rahisi ya uchepushaji maji kutoka mtoni kwa ajili ya kuzalisha mpunga.



Banio la jadi lililo jengwa kwa kutumia udongo na mawe

<i>Skimu ya jadi iliyo boreshwa</i>	Skimu iliyo anzishwa na kuendeshwa na wakulima wenyewe baada ya kupata msaada toka nje wa kujenga miundo mbinu ya kisasa.
<i>Skimu ya umwagiliaji ya kisasa</i>	Hii ni skimu ambayo imesanifiwa na kujengwa kitaalam, skimu za aina hii hujengwa na wahisani wa nje pamoja na michango au bila michango ya wakulima wafaidika. Katika skimu hizi uendeshaji wake unategemea zaidi misaada ya serikali au wahisani.
<i>Skimu za umwagiliaji kwa njia ya uvunaji maji</i>	Hii ni njia ambayo wakulima hutumia (ya majaruba) kuvuna maji ya mvua yanayosambaa juu ya ardhi na kuyahifadhi kwa kuzalisha mazao.

## 7. Aina ya skimu za umwagiliaji


<i>Nguvu ya Mteremko</i>	Skimu za umwagiliaji ambazo hugawa maji katika maeneo ya kilimo kwa kutumia nguvu ya mteremko.
<i>Pampu (mto)</i>	Skimu za umwagiliaji ambazo zenye chanzo cha maji ya mto ambazo maji huchukuliwa kwa njia ya kusukuma kwa pampu.
<i>Pampu (ziwa/dimbwi)</i>	Skimu za umwagiliaji ambazo chanzo chake cha maji ni ziwa/dimbwi na maji yake husukumwa kwa pampu.
<i>Uvunaji wa maji ya mvua</i>	Skimu za umwagiliaji ambazo wakulima hutumia mbinu rahisi katika maeneo yao ili kuhakikisha maji yanapatikana kwa ajili ya mazao. Uvunaji wa maji ya mvua katika mwongozo huu unajumuisha maji ya mafuriko katika skimu za umwagiliaji.
<i>Maji chini ya ardhi</i>	Skimu za umwagiliaji ambazo chanzo cha maji ni maji ya chini ya ardhi. Umwagiliaji kwa njia hii bado hauja ainishwa katika mwongozo huu, kwa sababu unahitaji uchunguzi maalum wa kihaidrolojia. Inashauriwa kupata ushauri toka umwagiliaji kanda, kama skimu zitaundwa kwa kutumia vyanzo vya maji kutoka chini ya ardhi.
<i>Bwawa</i>	Skimu za umwagiliaji ambazo chanzo cha maji ni mabwawa. Umwagiliaji wa mabwawa haujaainishwa katika mwongozo huu, kwa sababu unahitaji uchunguzi wa kiuhandisi. Inashauriwa kuunda skimu za umwagiliaji wa mabwawa kwa kupata ushauri toka ofisi ya umwagiliaji kanda.
<i>Pampu za miguu</i>	Hizi ni aina za pampu ambazo huchota maji kwa nguvu za mtumiaji kwa kutumia pedali. Pampu za miguu hazijaainishwa katika mwongozo huu, kwa sababu inatakiwa kuwekwa na wakulima wenyewe na sio serikali ya wilaya. Hata hivyo, uenezaji wa uwekaji wa pampu za miguu unawezwa kupendekezwa na DADP.

8. Kazi zinazinazo hitajika.	
<i>Ukarabati</i>	Ujenzi unafanywa ili kurudisha hali ya zamani ya skimu na kuhakikisha kuwa mifereji ya umwagiliaji na mifereji ya kutoa maji inafanya kazi bila kubadilisha mfumo wa umwagiliaji uliopo (sio kubadili umwagiliaji wa asili au iliyoboreshwa kuwa katika mfumo ya kisasa zaidi).
<i>Uboreshaji</i>	Ujenzi unafanywa ili kuhakikisha mifereji ya kutoa maji iliyopo inafanya kazi bila kubadilisha mfumo wa umwagiliaji (sio kubadili umwagiliaji wa asili au iliyoboreshwa kuwa katika mfumo ya kisasa zaidi).
<i>Maeneo mapya</i>	Ujenzi kwenye maeneo mapya ya umwagiliaji na kuweka mfumo ya mifereji ya kisasa .
<i>Kupanua eneo</i>	Ni kazi za uendelezaji kutoka kwenye maeneo yanayomwagiliwa mpaka sehemu zisizo fikiwa na miundombinu ya umwagiliaji.
<i>Mfumo wa kutolea maji mashambani</i>	Ni kazi za kuboresha mfumo wa kutolea maji mashambani kwa kujenga mfumo mpya au kuboresha uliopo bila kujenga mfumo wa umwagiliaji.

9. Usahili	
<i>Kaya</i>	Familia inayomilikiwa na mtu moja.
<i>Madhara yasiyo epukika</i>	Athari zinazoweza kutokea kutokana na kuendeleza umwagiliaji. Hizi ni athari za mazingira amabazo hazitokani na maendelo ya umwagiliaji. (kama vile mmomomyoko wa ardhi katika kilimo cha mvua)
<i>Migogoro ya maji ndani ya skimu/vijiji</i>	Ushindani wa matumizi ya rasilimali ya maji kati ya wanavijiji ndani ya skimu au katika kijiji husika.
<i>Migogoro ya maji kati ya skimu/kijiji</i>	Ushindani wa matumizi ya rasilimali ya maji kati ya wanavijiji, kati ya skimu au kati ya kijiji.
<i>Migogoro ya ardhi</i>	Ushindani wa matumizi ya rasilimali finyu ya ardhi kati ya wanavijiji au kati ya wakulima na wafugaji.

10. Vifaa	
<i>Kipima mahali kijiografia cha mkono (Handheld Global Positioning System "GPS")</i>	Kifaa hiki huainisha eneo kijiografia ili kupima sehemu kwa kutumia satalaiti. Ingawage makosa yanayofanywa na kifaa hiki katika kipimo cha mlalo ni kati ya mita 5 hadi 15, kwahiyosi vema kupima sehemu ndogo ndogo za eneo. Hata hivyo bado ni kizuri katika uanzishwaji wa skimu za umwagiliaji.
<i>Kifaa cha mkono cha mwendo wa umeme (Electrical Conductivity "EC")</i>	Kifaa hiki hupima kiwango cha chunvi katika maji ambacho ni kigezo muhimu katika kufahamu ubora wa maji. Kama kiwango cha chumvi katika maji ni kikubwa, kipimo cha chumvi kitaonyesha kuwa juu.





Kipima mahali kijiografia cha mkono (GPS)

Kifaa cha mkono cha mwendo wa umeme (EC Meter)

### 11. Mfumo wa takwimu

<p><i>Takwimu za umwagiliaji</i></p>	<p>Mfumo wa takwimu umeanzishwa hasa kwa ajili ya umwagiliaji katika idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi ya Wizara ya Kilimo na Chakula (KC). Hii ina kazi kuu tatu, kama vile 1) Kukagua maendeleo ya umwagiliaji, 2) Nyaraka za rejea, na 3) ramani ya maumbile ya ardhi. Takwimu na taarifa zilizo hifadhiwa kwenye mfumo wa takwimu zinaweza zikatumiwa na watumiaji wa miongozo kutokana na maombi yao kupitia kitengo cha takwimu na taarifa.</p>
<p><i>Mfumo wa habari wa kijiographia katika umwagiliaji (GIS)</i></p>	<p>Mfumo wa habari wa kijiographia (GIS) umeanzishwa hasa kwa ajili ya umwagiliaji katika idara ya umwagiliaji na huduma za kiufundi ya Wizara ya Kilimo na Chakula (KC). Hii iliandaliwa kwa madhumuni ya kuweza kusaidia kutathmini uwezo wa maeneo kwa ajili ya maendeleo ya umwagiliaji. Ina vipengele mbali mbali vya taarifa zenye kuainisha vitu kama mipaka ya kiutawala, mito na barabara pembezoni mwa kanda za ecojia za kilimo, hifadhi, maeneo ya uoto, kipande cha ardhi na aina ya udongo. Kwahiyo njia hii inaweza kutumika kwa ajili ya kutathimi maeneo mazuri ya umwagiliaji hasa sehemu zilizopendekezwa. Takwimu na taarifa zilizohifadhiwa kwenye GIS zinaweza kupewa watumiaji wa miongozo kutegemeana na maombi kupitia DI MU of DI TS.</p>

UTAYARI SHAJI  
WA  
MPANGO KABAMBE WA TAI FA WA UMWAGILIAJI  
KATIKA  
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**RASIMU YA MWONGOZO  
WA  
UANDAAJI WA MIRADI YA KILIMO CHA UMWAGILIAJI  
MAJI MASHAMBANI NDANI YA MPANGO WA  
MAENDELEO YA KILIMO YA WILAYA**

YALIYOMO

Matumizi ya Mwongozo  
Matumizi ya Maneno  
Orodha ya Vifupisho  
Vipimo

Ukurasa

<b>Sehemu ya 1 Utangulizi .....</b>	<b>1-1</b>
(1) Maelekezo .....	1-1
(2) Hali ya nyuma na madhumuni .....	1-1
(3) Taratibu zilizo pendekezwa kufuatwa katika kuendeleza skimu za umwagiliaji ya DADP .....	1-2
(4) Kanuni na taratibu muhimu .....	1-3
(5) Utaratibu wa kuandaa skimu za umwagiliaji .....	1-3
<b>Sehemu ya 2 Taratibu za kufuata kabla ya awamu ya DADP.....</b>	<b>2-1</b>
(1) Utangulizi .....	2-1
(2) Utaratibu wa maombi kwa serikali za wilaya.....	2-1
<b>Sehemu ya 3 Uandaaji wa skimu za umwagiliaji kwenye DADP.....</b>	<b>3-1</b>
Jinsi ya Kuendelea Hatua kwa Hatua.....	3-1
Hatua ya 1: Uthibitisho kama Uendelezaji wa Umwagiliaji ni Kipaumbele cha Wilaya.....	3-2
Hatua ya 2: Ukaguzi wa Haraka wa Skimu Zote za Umwagiliaji .....	3-4
Hatua ya 3: Uchambuzi/Mchujo wa Skimu Zote za Umwagiliaji.....	3-7
Hatua ya 4: Tathmini na Uidhinishaji kwa Kitengo cha Umwagiliaji cha Kanda .....	3-9
Hatua ya 5: Kazi ya Upimaji kwa Skimu Zilizochaguliwa.....	3-10
(a) Matayarisho Ofisini kabla ya kwenda Shambani.....	3-10
(b) Usaili wa Wadau.....	3-11
(c) Matayarisho ya Ramani ya Rasilimali za Kijiji.....	3-14
(d) Kufanya Makubaliano ya Eneo Lililopendekezwa .....	3-15

(e) Kuhakiki Hali ya Eneo .....	3-16
(f) Matayarisho ya Ramani ya Hali ya Sasa .....	3-22
<b>Hatua ya 6: Mpango wa Awali kwa Skimu za Umwagiliaji</b>	
<b>Zilizochaguliwa .....</b>	<b>3-24</b>
(a) Makadirio ya Mahitaji ya Maji kwa Umwagiliaji.....	3-24
(b) Uchunguzi wa Akiba ya Maji .....	3-28
(c) Mpango wa Undelezaji Skimu na Makadirio ya Gharama zake .....	3-32
(d) Makadirio ya Manufaa Yatakayo Ongezeka .....	3-41
(e) Mpango wa Kuendeleza Taasisi .....	3-44
(f) Masuala ya Mazingira .....	3-46
(g) Mapitio ya Mpango wa Undelezaji na Tathmini ya Kiuchumi ...	3-48
(h) Kutoa Kipaumbele kwa Skimu Zilizochaguliwa .....	3-50
<b>Hatua ya 7: Kutambua Programu za Ziada za Wilaya.....</b>	<b>3-54</b>
<b>Hatua ya 8: Usanifu wa Mpango wa Wilaya .....</b>	<b>3-56</b>
<b>Hatua ya 9: Namna ya Kutayarisha Taarifa ya Kuandaa Skimu.....</b>	<b>3-58</b>
<b>Hatua ya 10: Uhalalishaji na Makubaliano na Ofisi ya Umwagiliaji</b>	
<b>ya Kanda .....</b>	<b>3-60</b>
<b>Hatua ya 11: Warsha ya Mwitiko kwa Skimu Zilizochaguliwa .....</b>	<b>3-61</b>
<b>Hatua ya 12: Hitimisho la Mpango wa Kuanzisha Skimu ya</b>	
<b>Umwagiliaji .....</b>	<b>3-62</b>

**Sehemu ya 4 Mchakato wa kuendeleza umwagiliaji baada ya hatua ya DADP .....**

(1) Utangulizi/Jumla .....	4-1
(2) Njia ya kuendeleza skimu za umwagiliaji baada ya uchaguzi.....	4-1
(3) Uongozi wenye kuhiari mchakato ya maendeleo.....	4-2

**Sehemu ya 5 Matumizi ya takwimu katika kuandaa skimu za umwagiliaji .....**

(1) Utangulizi .....	5-1
(2) Takwimu muhimu zinatikane kutoka mfumo wa takwimu zilizohifadhiwa .....	5-1
(3) Taarifa ya uwasilishaji wa matokeo ya kuandaa mpango kwenye kitengo cha takwimu .....	5-1
(4) Mfumo wa utunzaji takwimu .....	5-2

ORODHA YA FOMU

Ukurasa

Fomu kwaajili ya ukaguzi wa haraka na uchambuzi

Fomu Na-1	Orodha ya Skimu za Umwagiliaji katika Wilaya .....	3-3
Fomu Na-2	Karatasi ya Upimaji ya Ukaguzi wa Haraka wa Eneo .....	3-5

Fomu kwaajili ya mipango ya awali na utoaji wa kipaumbele

Fomu Na-3	Karatasi ya Upimaji kwa Ajili ya Usaili wa wadau.....	3-12
Fomu Na-4	Karatasi ya Upimaji kwa Kuthibitisha Hali ya Eneo .....	3-17
Fomu Na-5	Karatasi ya Kukokotoa Mahitaji ya Maji ya Umwagiliaji.....	3-25
Fomu Na-6	Karatasi ya Kukokotoa Uchunguzi wa Wingi wa Maji.....	3-29
Fomu Na-7	Karatasi ya Mpango kwenye Mpango wa Uendelezaji wa Skimu .....	3-33
Fomu Na-8	Karatasi ya Kukadiria Manufaa Yatakayo Ongezeka Kutokana na Skimu .....	3-42
Fomu Na-9	Karatasi ya Mpango kwa Ajili ya Mpango wa Kuendeleza Taasisi .....	3-45
Fomu Na-10	Taarifa za Nyongeza kuhusu Mazingira .....	3-47
Fomu Na-11	Maswali ya Mpango wa Kuendeleza Skimu ya Umwagiliaji .....	3-49
Fomu Na-12	Karatasi ya Kupanga Kipaumbele .....	3-51
Fomu Na-13	Muhtasari wa skimu (Muhtasari wa Mpango wa awali wa DADPs) ....	3-52
Fomu Na-14	Muhtasari wa Mpango wa Ziada wa Wilaya.....	3-57
Fomu Na-15	Muhtasari wa Mpango wa Kuanzisha Skimu za Umwagiliaji .....	3-59

ORODHA YA VI AMBATANI SHO

Kiambatanisho-1	Miongozo na Taratibu Muhimu.....	AT1-1
1	Mwongozo wa mpango wa maendeleo ya kilimo katika wilaya DADPs .....	AT1-1
2	Mwongozo na taratibu katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji .....	AT1-3
(1)	Mwongozo Shirikishi katika Uboreshaji wa Miradi Midogomidogo ya Umwagiliaji I liyoanzishwa na Kusimamiwa na Wakulima, Julai 2003 .....	AT1-3
(2)	Mwongozo wa Kupanga Kuandaa Miradi ya Umwagiliaji .....	AT1-4
(3)	Mwongozo wa Kusanifu Miradi ya Umwagiliaji .....	AT1-4
(4)	Mwongozo wa Kusanifu Miradi ya Umwagiliaji kwa Njia ya Uvunaji Maji ya Mvua katika Maeneo yenye Ukame .....	AT1-5
(5)	Mwongozo wa Matumizi Bora ya Maji katika Kilimo cha Umwagiliaji kwa Maafisa Ugani .....	AT1-5
Kiambatanisho-2	Muhtasari wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji .....	AT2-1
Kiambatanisho-3	Maelezo ya Ziada juu ya Uchambuzi Kiuchumi wa Skimu.....	AT3-1

## ORODHA YA VIFUPI SHO

ASDP	Agricultural Sector Development Programme <i>(Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo)</i>
ASDS	Agricultural Sector Development Strategy <i>(Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo)</i>
DADP	District Agricultural Development Plan <i>(Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya)</i>
DALDO	District Agriculture and Livestock Development Officer <i>(Afisa Kilimo/Mifugo wa Wilaya)</i>
DASAC	District Agricultural Sector Advisory Committee <i>(Kamati ya Ushauri wa Kilimo ya Wilaya)</i>
DED	District Executive Director <i>(Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)</i>
DI MU	Data and Information Management Unit <i>(Kitengo cha Usimamizi wa Takwimu na Taarifa)</i>
DI TS	Division of Irrigation and Technical Service <i>(Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi)</i>
DPDT	District Project Development Team <i>(Timu ya Wilaya ya Kuendeleza Mradi)</i>
EC	Electric Conductivity <i>(Mwendo wa Umeme Majini)</i>
EIA	Environmental Impact Assessment <i>(Tathmini ya Athari za Mazingira)</i>
ESA	Environmental Sensitive Areas <i>(Sehemu Nyeti za Mazingira)</i>
ETo	Evapo-Transpiration <i>(Uvukizwaji wa maji aridhini na kwenye mmea)</i>
GIS	Geographic Information System <i>(Mfumo wa Jiografia wa kupata taarifa)</i>
GPS	Global Positioning System <i>(Mfumo wa kuonyesha mahali kitu/mtu kilipo/alipo duniani)</i>
IA	Irrigators' Association <i>(Umoja wa Wamwagiliaji)</i>
IRR	Internal Rate of Return <i>(Kipimo cha kuonyesha Urejeshaji wa mtaji)</i>
JICA	Japan International Cooperation Agency <i>(Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japani)</i>
MAFS	Ministry of Agriculture and Food Security <i>(Wizara ya Kilimo na Chakula)</i>
NEMC	National Environmental Management Council <i>(Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira)</i>
NGO	Non-Government Organization <i>(Shirika lisilokuwa la Kiserikali)</i>
NI MP	National Irrigation Master Plan <i>(Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji)</i>
O&OD	Opportunities and Obstacles to Development <i>(Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (Mpango wa Kijiji))</i>
SMS	Subject Matter Specialist <i>(Mtaalam wa fani husika k.m. Umwagiliaji, Kilimo n.k.)</i>
ZIU	Zonal Irrigation Unit <i>(Kitengo cha Umwagiliaji cha Kanda)</i>
ZRC	Zonal Review Committee

*(Kamati ya 'mapitio' ya Kanda)*

**VIPIMO**

**Extent (*Ukubwa*)**

cm<sup>2</sup> = Square-centimeters (1.0 cm x 1.0 cm)  
m<sup>2</sup> = Square-meters (1.0 m x 1.0 m)  
Km<sup>2</sup> = Square-kilometers (1.0 km x 1.0 km)  
ha = Hectares (10,000 m<sup>2</sup>)  
ac = Acres (4,046.8 m<sup>2</sup> or 0.40468 ha.)

**Length (*Urefu*)**

mm = Millimeters  
cm = Centimeters (cm = 10 mm)  
m = Meters (m = 100 cm)  
km = Kilometers (km = 1,000 m)

**Currency (*Fedha*)**

Tsh = Tanzanian Shillings

**Volume (*Ujazo*)**

cm<sup>3</sup> = Cubic-centimeters  
= (1.0 cm x 1.0 cm x 1.0 cm or 1.0 m-lit.)  
m<sup>3</sup> = Cubic-meters  
= (1.0 m x 1.0 m x 1.0 m or 1.0 k-lit.)  
lit (l) = Liter (1,000 cm<sup>3</sup>)

**Weight (*Uzito*)**


gr = Grams  
kg = Kilograms (1,000 gr.)  
ton = Metric ton (1,000 kg)

**Time (*Muda*)**

sec = Seconds  
min = Minutes (60 sec.)  
hr = Hours (60 min.)

# Sehemu ya 1

## Utangulizi





---

## Sehemu ya 1 Utangulizi

### (1) Maelekezo

Mwongozo huu ni tafsiri kutoka katika nakala halisi ya kiingereza, kama kutakuwa na sehemu ambayo tafsiri yake haileweki vizuri wakati wa matumizi ni vema kufanya marejeo katika nakala halisi ya kiingereza.

Mwongozo huu ulitayarishwa kama sehemu ya uhakiki utafiti wa Mkakati Kabambe wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji ndani ya jamhuri ya Tanzania, kama ilivyo ainishwa katika ujumla wa kazi baina ya Wizara ya Kilimo na Chakula, ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (MAFS) na Shirika la Maendeleo ya kimataifa la Japani (JICA) mnamo April 10, 2001.

### (2) Hali ya nyuma na madhumuni

#### (a) Hali ya nyuma

Mpango Kabambe wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Kitaifa unasisitiza kuwa mafanikio na maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji yanategemea ufanisi katika nyanja zote zinazo husika katika, kilimo cha umwagiliaji kama vile kupanga mipango bora, usanifu na ujenzi mzuri pamoja na uendeshaji na utunzaji. Katika utaratibu huu, ni muhimu wakati wa kuandaa mpango wa kilimo cha umwagiliaji uchaguzi wa skimu sahihi iwe ni shughuli muhimu ya awali ambayo itapelekea utekelezaji wake uwe wa mafanikio.

Skimu nyingi za umwagiliaji zilizokaguliwa wakati wa utayarishaji wa Mpango Kazi wa Upembuzi, zilionyesha kuwa mikakati iliyokuwa nayo katika kuendeleza skimu ilikuwa haifahamiki sawa sawa na watumishi wa wilaya hususan katika kipengele kinachohusu utaalamu wa kiufundi pamoja na uchambuzi wa kiuchumi. Pia hakukuwa na vigezo vilivyo wazi ambavyo vilitumika katika uchaguzi wa skimu za umwagiliaji katika mipango ya vijiji.

Ili kuboresha hali hii, ilibainisha kuwa ni muhimu kutayarisha na kutumia mwongozo wa vitendo ambao unaonyesha taratibu za kufuatwa kwa mtiririko wakati wa kuandaa skimu ambazo zitaorodheshwa katika DADP. Mafunzo juu ya matumizi ya mwongozo yatahitajika kwa watumishi watacao husika katika ngazi ya wilaya ili uweze kutumiwa ipasavyo.

Mkakati wa programu fupi (2003 hadi 2007) chini ya Programu ya Maendeleo ya kufikia mwaka 2017, ni kubadilisha hali iliyopo kwa kuzipa nguvu zaidi wilaya katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Hivyo matayarisho ya mwongozo huu na utoaji wa mafunzo katika ngazi ya wilaya kama ilivyobainishwa hapo juu unawiana na dhana ya mkakati katika kufikia lengo.

**(b) Madhumuni**

Madhumuni ya mwongozo huu ni kuwapa wataalamu wa wilaya taratibu za kuandaa skimu za umwagiliaji maji katika utayarishaji wa DADP; taratibu zake zinahusu ukaguzi wa haraka wa eneo, uchambuzi, upembuzi wa awali, kuweka kipaumbele, kutathmini na kuchagua shughuli za utekelezaji.

**(3) Taratibu zilizo pendekezwa kufuatwa katika kuendeleza skimu za umwagiliaji ya DADP**

Katika sehemu hii, utaratibu mzima wa kuendeleza skimu za umwagiliaji umefafanuliwa ili kubainisha taratibu za kuandaa skimu za umwagiliaji kwa ajili ya DADPs. Utaratibu mzima unapaswa kutayarishwa kulingana na taratibu zilizopo, kama vile Taratibu za Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya, Novemba 2003 (angalia **Kiambatanisho-1**), na Mbinu Shirikishi katika Kuboresha Kilimo cha Umwagiliaji wa Wakulima Wadogowadogo wa Skimu za Umwagiliaji Walizozianzisha na Kuziendesha wa Wenyewe, Julai 2003 (angalia **Kiambatanisho-1**). Kwa nyongeza, taratibu zote kwa ujumla zinapaswa kuwa na dhana ya kuhitaji kutoka kwa wakulima kwa njia ya ushirikishwaji. Kufuatana na maelezo ya hapo juu, utaratibu wa kuendeleza skimu za umwagiliaji chini ya DADPs umepangwa katika dhana kuu muhimu kama zifuatavyo:


- Orodha ya skimu za umwagiliaji ambazo zimetokana na dhana ya hitaji toka kwa walengwa.

Maombi yote ya kuendeleza skimu za umwagiliaji yanapaswa kutoka katika serikali za vijiji na kuonyesha hitaji halisi la wakulima limezingatiwa. Kufuatana na agizo la serikali, matumizi ya taratibu za DADP zinabainisha wazi kuwa kwa kutumia njia ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo kama mbinu mahususi katika kuandaa mpango shirikishi imeonyesha kuwa na mafanikio (njia hii imeonyeshwa sehemu ya 3). Hivyo, inapaswa kutiliwa maanani wakati wa kuandaa skimu za umwagiliaji chini ya utaratibu wa DADP

- Maendeleo ya skimu za umwagiliaji katika Serikali za Wilaya zinapaswa Kushirikisha Wakulima

Maendeleo ya skimu za umwagiliaji yanapaswa kufanywa kwa kufuata mbinu shirikishi ambayo itawashirikisha wakulima wote, ili kuwajengea ufahamu na umilikishwaji wa skimu za umwagiliaji ndani yao, sambamba na mbinu za ushirikishwaji, Wizara ya Kilimo na Chakula imetayarisha Taratibu za Mbinu Shirikishi katika kuboresha Kilimo cha Umwagiliaji wa Wakulima Wadogo wadogo wa Skimu za Umwagiliaji Walizozianzisha na Kuziendesha wa Wenyewe, Julai 2003 chini ya ASPs. Hivyo basi, taratibu za kuandaa skimu za umwagiliaji kwa ajili ya DADPs utafafanuliwa katika mwongozo huu.

Jedwali lifuatalo linaonyesha mapendekezo ya hatua katika maendeleo ya skimu za umwagiliaji chini ya DADPs:



Katika hatua hizi, lengo kuu ni kuandaa skimu ya umwagiliaji.

#### (4) Kanuni na taratibu muhimu

Kuna aina nyingi za taratibu na kanuni katika Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula ambazo zimetayarishwa na miradi tofauti kulingana na matakwa ya mradi husika. Nayo ni kama ifuatavyo:


- Mwongozo shirikishi katika uboreshaji wa miradi midogo ya umwagiliaji iliyoanzishwa na kusimamiwa na wakulima, Julai 2003
- Mwongozo wa kupanga miradi ya umwagiliaji
- Mwongozo wa kusanifu miradi ya umwagiliaji
- Mwongozo wa kusanifu miradi ya uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yenye ukame
- Mwongozo wa matumizi bora ya maji ya umwagiliaji kwa wataalamu wa ugani

Kwa watumishi katika ngazi ya wilaya, taarifa na marejeo juu ya vipengele muhimu za taratibu na kanuni zimeelezwa kwa ufupi kwenye **Kiambatanisho-1**.

#### (5) Utaratibu wa kuandaa skimu za umwagiliaji

Utaratibu wa kuandaa skimu za umwagiliaji umeonyeshwa katika jedwali lililopo katika ukurasa unaofuata.

## UTARATIBU WA KUANDAA SKIMU



*Sehemu ya 2*  
*Taratibu za kufuata*  
*kabla ya awamu ya DADP*



## Sehemu ya 2      Taratibu za kufuata kabla ya awamu ya DADP

### (1) Utangulizi


Kama ilivyoainishwa katika sehemu ya utangulizi, skimu zote zinazotakiwa kuendelezwa, zinapaswa kutuma maombi kwa kufuata utaratibu ufuatao. Wana kijiji husika watume maombi yao kupitia serikali ya kijiji ambayo yatapitishwa na kamati ya maendeleo ya kata na hatimaye kuwasilishwa katika serikali ya wiliya (utaratibu huu unaitwa uandaaji wa mpango toka ngazi ya chini) ili kufanikisha njia hii katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa utaratibu wa kutayarisha mpango toka chini, mwongozo wa DADP unapendekeza matumizi ya fursa na vikwazo katika maendeleo kama njia sahihi ya mpango shirikishi ambayo imekubalika na serikali. Taratibu za kuunda skimu za umwagiliaji kwa ajili ya DADPs, zifuate taratibu hizo hizo katika kupata skimu za umwagiliaji kulingana na matakwa ya wananchi husika.

### (2) Utaratibu wa maombi kwa serikali za wilaya

Taratibu za maombi ya maendeleo ya skimu za umwagiliaji kutoka kwa wakulima zinatakiwa kuwiana na "TARATIBU ZA UANDAAJI MPANGO SHIRIKISHI JAMII KWA KUTUMIA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO, April 2002" pamoja na taratibu za mpango wa maendeleo ya kilimo ya wilaya, Novemba 2003. Utaratibu wa maombi kutoka katika aina hizi mbili za miongozo umegwanyika katika makundi makuu matatu: 1. Mkutano wa uzinduzi, 2. Kutayarisha mpango wa kijiji, 3. Kuandaa mpango ambao shughuli muhimu zimeainishwa katika jedwali la kulia.

Mipango ya maendeleo ya kijiji na kata pamoja na shughuli za umwagiliaji itajumuisha pia sekta nyingine muhimu kama vile afya, elimu, barabara, masoko n.k. Skimu zilizopewa kipaumbele zitachaguliwa miongoni mwao kwa kufuata dira ya wilaya pamoja na malengo ya ASDP na ASDS.

#### Utaratibu maombi ya kuendeleza



## Sehemu ya 3

*Uandaaji wa skimu za  
umwagiliaji kwenye DADP*



Sehemu ya 3 Uandaaji wa skimu za umwagiliaji kwenye DADP

Jinsi ya Kuendelea Hatua kwa Hatua

**1. Muundo Mkuu**

Sehemu kubwa ya mwongozo (Sehemu ya 3: Uundaji wa skimu za umwagiliaji kwenye DADP) inaelezwa katika muundo ufuatao. Tazama maelezo yafuatayo ili kuelewa zaidi.

**Muundo Mkuu**

**Jina la Hatua ya 1**

Jambo Muhimu  
Maneno muhimu kwa hatua ya -1

*1. Kwanza, soma kwa makini "Jambo Muhimu", "Kwa nini kazi inahitajika?", na "Namna ya kufanikisha kazi" ili kuifahamu vema hatua ya -1.*

Kwa nini kazi inahitajika?  
Maelezo yanayoonyesha umuhimu wa hatua ya -1

Namna ya kufanikisha kazi  
Maelezo ya namna ya kufikia malengo ya hatua ya -1

Yanayohitajika  
Maelezo ya vitu vinavyohitajika katika hatua ya -1, kama timu ya watekelezaji, vifaa, na taarifa na habari muhimu.

Namna gani kazi inafanyika?  
*2. Kisha, soma "Yanayohitajika" na hakikisha nani anahusika katika hatua ya -1. Kama kuna vifaa vinahitajika n.k., hakikisha unavyo kabla ya kuanza hatua ya -1.*

*3. Hatimaye, chukua hatua kulingana na mlongo wa maelezo ya "Namna gani kazi inafanyika?".*

Hatua ndogo ya 1	Jina la hatua ndogo ya 1	Maelezo ya utaratibu katika hatua ndogo ya 1.
Hatua ndogo ya 1	Jina la hatua ndogo ya 1	Maelezo ya utaratibu katika hatua ndogo ya 2

**2. Viashiria vya Utendaji Kazi**

Si lazima kufanya kazi katika hali fulani kwa mfano, vipimo vya ujazo wa ziwa/dimbwi si lazima ikiwa chanzo cha maji si ziwa/dimbwi. Endapo utakuta kiashirio kifuatacho, hakikisha kama kazi inahitajika au la kabla ya kuanza kazi inayokusudiwa.

**Kiashirio cha Utekelezaji Kazi**

Hatua ndogo ya 1	Jina la hatua ndogo ya 1
<u>Matumizi</u>	Hatua ndogo hii itumike kwenye skimu ambazo zina duara
1) Aina ya Umwagiliaji	
<input type="checkbox"/> Mtiririko wa Maji	<input type="checkbox"/> Pampu (Ziwa/Dimbwi)
2) Aina ya Kazi za Kuendeleza Umwagiliaji	
<input type="checkbox"/> Ukarabati	<input type="checkbox"/> Uboreshaji
<input type="checkbox"/> Maeneo Mapya	<input type="checkbox"/> Upanuzi
<input type="checkbox"/> Utoaji Maji	

*Kama hakuna duara, kazi si lazima kufanyika. Katika mfano huu, skimu ya pampu (ziwa/dimbwi) au ya kutoa maji mashambani si muhimu.*



## Hatua ya 1: Uthibitisho kama Uendelezaji wa Umwagiliaji ni Kipaumbele cha Wilaya

### Jambo Muhimu

Hakikisho kutoka wilayani kuwa umwagiliaji ni kipaumbele na unaendana na hali ya wilaya na Mpango Kamambe wa Taifa wa Umwagiliaji.

### Kwa nini kazi inahitajika?

Ukipaumbele wa skimu za umwagiliaji ufanywe kulingana na mipango ya uendelezaji umwagiliaji wa wilaya (mwelekeo wa uendelezaji wa umwagiliaji wa wilaya).

### Namna ya kufanikisha kazi

Kuna haja ya kutathmini hali halisi ya wilaya na mwelekeo wa wilaya katika masuala ya uendelezaji wa umwagiliaji kwa kuzingatia Mpango wa Taifa wa Umwagiliaji.

### Yanayohitajika

1. Timu ya Wilaya ya Kuendeleza Mradi (DPDT)
2. Muhtasari wa Mpango Kamambe wa taifa wa Umwagiliaji (NIMP) (angalia Kiambatanisho-2)
3. Taarifa ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP).
4. Taarifa ya Mipango ya Kuendeleza Kilimo ya Wilaya (DADPs).
5. Fomu ya orodha ya skimu za umwagiliaji wilayani (Fomu Na-1)

### Namna gani kazi inafanyika?

Hatua ndogo ya 1 Andaa Timu ya Uendelezaji Mradi ya Wilaya.	Timu ya Wilaya ya Kuendeleza Mradi (DPDT) itaundwa na Mtaalam wa Umwagiliaji wa wilaya (SMS), Mtaalam wa Kilimo wa wilaya (SMS), afisa Ugani na wataalam wengine muhimu katika ofisi ya wilaya.
Hatua ndogo ya 2 Matayarisho ya orodha ya skimu za umwagiliaji katika wilaya.	Angalia Fomu Na-1. Hii itakuwa ni orodha ya msingi ya skimu za umwagiliaji wilayani. Ni muhimu kuonyesha kila skimu iko katika hatua gani na ina eneo kiasi gani linalomwagiliwa. Hakuna haja ya kufanya tathmini ya haraka kwa skimu ambazo tayari zimekamiliwa na hazihitaji kazi zaidi.
Hatua ndogo ya 3 Mapitio ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP).	Fanya mapitio ya ASDP na thibitisha jukumu la ukuaji wa sekta ndogo ya umwagiliaji kulingana na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo.
Hatua ndogo ya 4 Mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Kuendeleza Umwagiliaji (NIMP).	Fanya mapitio ya NIMP na thibitisha jukumu la wilaya katika kuendeleza umwagiliaji nchini ili kufikia lengo lililoainishwa katika Mpango Kabambe (angalia Kiambatanisho-2).
Hatua ndogo ya 5 Fanya tathmini ya hali ya sasa ya shughuli za umwagiliaji katika wilaya.	Fanya tathmini ya hali halisi ya shughuli za umwagiliaji kwa kuangalia kwa makini Fomu Na-1. Matatizo na vikwazo vinavyokwamisha maendeleo ya umwagiliaji katika wilaya yatabainishwa na hatua za udhibiti zitafafanuliwa.
Hatua ndogo ya 6 Tayarisha kipaumbele cha uendelezaji umwagiliaji katika Wilaya.	Mwelekeo wa siku za usoni wa kuendeleza umwagiliaji ni bora ukawekwa bayana kama kipaumbele cha wilaya kwa kuzingatia vikwazo na ufumbuzi kama ilivyoelezwa hapo juu. Wajumbe wa DPDT wanatakiwa kufikia muafaka wa kipaumbele cha uendelezaji wa umwagiliaji katika wilaya.

Fomu Na-1 Orodha ya Skimu za Umwagiliaji katika Wilaya

Jina la Wilaya \_\_\_\_\_

Imetayarishwa (Tarehe na Mwaka) \_\_\_\_\_

Imetayarishwa na \_\_\_\_\_

Na.	Jina la Skimu	Kata	Kijiji/Vijiji	Hatua ya Maendeleo (zungushia mojawapo ya hatua)	Eneo linalomwagiliwa kwa sasa	Ukaguzi wa Haraka kwa Eneo Husika
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi
				O&OD, DADP, F/S, D/D, Ujenzi, Kumaliza ujenzi	ha	Unatakiwa Hautakiwi

Kumbuka: O&OD: Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (au Mpango wa Kijiji), DADP: Mipango ya Kuendeleza Kilimo ya Wilaya, F/S: Upembuzi Yakunifu, D/D: Usanifu Kamili

- Endapo skimu iliyoteuliwa iko katika hatua ya O&OD (Mpango wa Kijiji), ukaguzi wa haraka wa eneo husika hapana budi ufanyike.
- Orodha iliyotayarishwa iwasilishwe katika ofisi ya umwagiliaji ya kanda pamoja na taarifa ya ukaguzi wa haraka wa eneo husika na taarifa ya mchujo.

## Hatua ya 2: Ukaguzi wa Haraka wa Skimu Zote za Umwagiliaji

### Jambo Muhimu

Thibitisha hali ya sasa ya skimu ya umwagiliaji kwa kutumia habari muafaka na adidu za rejea.

### Kwa nini kazi inahitajika?

Ili kufanikiwa katika mipango ya kuendeleza umwagiliaji katika kipindi kifupi, kuna haja ya kuhakiki ubora wa taarifa za umwagiliaji zilizoko katika Mpango wa Kata.

### Namna ya kufanikisha utekelezaji

Katika hatua hii, si lazima kufanya ukaguzi wa kina wa eneo. Ukaguzi ufanyike ili kujua kama kweli kuna skimu za umwagiliaji zenye hali kama inavyoonyeshwa katika Mpango wa Kata. Kwa madhumuni haya, karatasi ya upimaji ni ya muhimu sana kujazwa ili kupata taarifa sahihi.

### Yanayohitajika

1. Timu ya Wilaya ya Kuendeleza Mradi (DPDT)
2. Karatasi ya Upimaji kwa ajili ya Ukaguzi wa Haraka wa Eneo (Fomu Na-2)
3. Kionyesha mahali cha mkononi (GPS) na Kifaa cha Kupima Mwendu wa Umeme Majini (EC meter)
4. Kamera (kama inapatikana)

### Namna qani kazi inafanyika?

Hatua Ndogo ya 1 Fanya matayarisho kabla ya kutembelea maeneo.	1) Pata taarifa muhimu za awali kutoka katika kitengo cha Kuhifadhi takwimu na taarifa cha DITS, Wizara ya Kilimo na Chakula (kama matokeo ya upimaji, aina ya udongo, kifuniko cha ardhi, kanda ya hali ya hewa na kilimo, eneo la hifadhi, ramani za mwinuko na mwanguko katika skeli ya 1:50,000. 2) Uwe na GPS na Kifaa cha Kupima Mwendu wa Umeme Majini. 3) Fanya mawasiliano ya awali kuhusu Hati Miliki ya Maji kwa upande wa chini wa mfereji, kwenye ofisi husika ya maji. 4) Tayarisha ratiba ya ukaguzi wa eneo husika. 5) Toa taarifa kwa wenyeviti wa vijiji husika kuhusu ratiba ya zoezi la ukaguzi wa haraka kwa maeneo husika na waombe wawaalike wadau kama wenyeviti wa umoja wa umwagiliaji na baadhi ya wanavijiji.
Hatua ndogo ya 2 Tembelea eneo la skimu.	Tembelea eneola skimu kulingana na ratiba iliyoandaliwa ya ukaguzi wa eneo.
Hatua ndogo ya 3 Fanya usaili kwa wanakijiji.	Kusanya watu husika kama mwenyekiti wa kijiji, mwenyekiti wa umoja wa umwagiliaji na wakulima. Fanya usaili kwa kutumia karatasi ya upimaji.
Hatua ndogo ya 4 Kagua eneo linalofaa kwa umwagiliaji (au eneo linalomwagiliwa kwa sasa).	Tembelea eneo linalofaa kwa umwagiliaji (au linalomwagiliwa kwa sasa) pamoja na wanakijiji husika. Kusanya takwimu zaidi katika eneo husika na hakiki taarifa zilizopatikana kwenye usaili. Pima kwa kutumia GPS ili kujua mahali halisi eneo lilipo (GPS inapatikana katika kila ofisi ya umwagiliaji ya kanda).
Hatua ndogo ya 5 Kagua chanzo cha maji cha skimu husika.	Tembelea chanzo cha maji cha skimu kwa pamoja na wanakijiji. Pima ubora wa maji kwa kutumia kipima mwendo wa umeme katika maji (EC meter). Kusanya taarifa zaidi kuhusu hali ya mafuriko na ukame na jaribu kuelewa kama rasilimali ya maji inaweza kutosheleza kwa eneo linalofaa kwa umwagiliaji.
Hatua ndogo ya 6 Kamilisha kujaza karatasi ya upimaji na kagua kama taarifa ni za kuaminika.	Ukaguzi ili kujua kama taarifa ni zakuaminika hapana budi ufanyike kwenye eneo husika ili kuepuka ukaguzi zaidi kadri inavyowezekana.

**Kumbuka:** Zoezi la ukaguzi wa haraka wa eneo linakadiriwa kukamilika katika muda wa saa 1-2 kwa skimu (muda huu hauhusishi muda wa kusafiri).

Fomu Na-2 Karatasi ya Upimaji ya Ukaguzi wa Haraka wa Eneo (1/2)

1. Taarifa za Ujumla	Tarehe ya Upimaji
(1) Jina la Skimu :	_____
(2) Ilipo (sehemu yoyote katika skimu) : Latitudo: _____ Longitudo: _____	
(3) Utawala : Kata _____	
: Kijiji/Vijiji _____	
(4) Idadi ya Kaya : _____ kaya/ _____	
2. Hali ya Sasa ya Eneo lifaalo kumwagiliwa (wanakijiji wasailiwe na kuhakiki kwa kutembelea eneo husika)	
2.1 Hali ya Sasa ya Kilimo Katika Eneo Linalofaa Kumwagiliwa	
(1) Hali ya sasa : <input type="checkbox"/> Halijalimwa <input type="checkbox"/> Limelimwa ( _____ ha kwa mwaka)	
(2) Mazao yaliyopo : <input type="checkbox"/> Mpunga <input type="checkbox"/> Mahindi <input type="checkbox"/> Mbogamboga <input type="checkbox"/> Mengine ( _____ )	
(3) Masoko yaliyopo : _____ ( _____ km kutoka kwenye eneo)	
(4) Tatizo la kutuama maji : <input type="checkbox"/> Hakuna tatizo <input type="checkbox"/> Lipo kiasi fulani <input type="checkbox"/> Lipo sana	
(5) Mafuriko : <input type="checkbox"/> Si sana <input type="checkbox"/> Mara moja kwa mwaka <input type="checkbox"/> Zaidi ya mara mbili kwa mwaka	
2.2 Mfumo wa Umwagiliaji Uliopo	
(1) Mfumo wa umwagiliaji kwa sasa : <input type="checkbox"/> Wa asili <input type="checkbox"/> Wa asili ulioboresywa	
<input type="checkbox"/> Wa kisasa <input type="checkbox"/> Uvunaji maji ya mvua <input type="checkbox"/> Hakuna umwagiliaji	
(2) Eneo linalomwagiliwa kwa sasa : _____ ha (kama skimu tayari inamwagiliwa)	
(3) Chanzo kikuu cha maji : <input type="checkbox"/> Mto wa kudumu <input type="checkbox"/> Mto wa msimu <input type="checkbox"/> Ziwa/Dimbwi	
<input type="checkbox"/> Maji ya chini ya ardhi <input type="checkbox"/> Chemchemu <input type="checkbox"/> Uvunaji maji ya mvua	
(4) Jina la chanzo cha maji : _____	
2.3 Umoja wa Wamwagiliaji (IA) Uliopo au Kikundi Kinachofanya Shughuli Zinazohusiana na Umwagiliaji	
(1) Uundaji wa IA : <input type="checkbox"/> Umeundwa mwaka _____ <input type="checkbox"/> Haujaundwa	
(2) Jina la umoja : _____	
(3) Mwaka wa usajili : _____	
(4) Idadi ya wanachama : _____	
2.4 Uendelezaji wa Umwagiliaji Unaofanywa kwa Sasa na Serikali au Shirika Jingine	
(1) Aina ya msaada : <input type="checkbox"/> Vifaa vya Umwagiliaji <input type="checkbox"/> Mengineyo ( _____ ) <input type="checkbox"/> Hakuna	
3. Mpango Uliopendekezwa na Kijiji kwa kutumia O&OD n.k.(mpango uliopendekezwa na kijiji)	
3.1 Mpango wa uendelezaji Mfumo wa Umwagiliaji	
(1) Eneo linalofaa kumwagiliwa : _____ ha	
(2) Chanzo kikuu cha maji : <input type="checkbox"/> Mto wa kudumu <input type="checkbox"/> Mto wa msimu <input type="checkbox"/> Ziwa/dimbwi	
<input type="checkbox"/> Maji ya chini ya ardhi <input type="checkbox"/> Chemchemu <input type="checkbox"/> Uvunaji maji ya mvua	
(3) Jina la chanzo cha maji : _____	
(4) Hati ya kumiliki maji : <input type="checkbox"/> Imetolewa <input type="checkbox"/> Bado haijatolewa <input type="checkbox"/> Inatarajiwa <input type="checkbox"/> Haijulikani	
(5) Kazi zinazohitajika : <input type="checkbox"/> Ukarabati <input type="checkbox"/> Eneo jipya	
<input type="checkbox"/> Uboreshaji (kutoka asili kwenda kisasa) <input type="checkbox"/> Uboreshaji utoaji maji	
(6) Aina ya umwagiliaji : <input type="checkbox"/> Mtiririko <input type="checkbox"/> Pampu <input type="checkbox"/> Pampu ya miguu <input type="checkbox"/> Uvunaji maji ya mvua	
(7) Ubora wa maji (EC) : <input type="checkbox"/> Kiwango cha juu $EC \geq 2.25$ mS/cm <input type="checkbox"/> Kiwango kisicho cha juu $EC < 2.25$ mS/cm	
	(hayafai kwa umwagiliaji)

**Fomu Na-2 Karatasi ya Upimaji ya Ukaguzi wa Haraka wa Eneo (2/2)**

3.2 Mpango wa Kuendeleza Kilimo

(1) Mazao yanayopendekezwa :  Mpunga  Mahindi  Mbogamboga  Mengine ( )

(2) Masoko yanayopendekezwa : Jina ( km kutoka eneo husika)

3.3 Mpango wa Kuanzisha Umoja wa Wamwagiliaji

(1) Mpango wa Uanzishaji :  Umeanzishwa  Utaanzishwa mwaka .....  Hakuna Uhakika

(2) Namna ya kuchangia maendeleo :  Pesa taslimu  Nguvu zao  Hakuna

4. Athari Mbaya Zinazotarajiwa

Migogoro ya matumizi ya maji kwenye skimu/kijijini  Migogoro ya matumizi ya maji na skimu/kijiji kingine

Mgogoro wa ardhi  Kuingilia maeneo ya hifadhi  Mmomonyoko wa udongo katika skimu

Chanzo cha mgogoro ( )

5. Maoni ya Timu ya Ukaguzi

(1) Motisha ya wakulima kuhusu umwagiliaji :  Iko juu  Ni ya wastani  Iko chini

(2) Hali ya msaada kwenye skimu kwa sasa :  Unatosha  Msaada zaidi unahitajika  Hakuna msaada

6. Maoni ya viongozi wa kijiji na walengwa

7. Historia ya Skimu

8. Mambo Yaliyogunduliwa na Timu ya Maendeleo ya Wilaya

### Hatua ya 3: Uchambuzi/Mchujo wa Skimu Zote za Umwagiliaji

**Jambo Muhimu**

Uchambuzi wa skimu za umwagiliaji kwa kuzingatia vigezo sahihi na uwazi chini ya umiliki wa Serikali katika ngazi ya wilaya.

**Kwa nini kazi hii inahitajika?**

Si rahisi kupanga kuendeleza skimu zote za umwagiliaji zilizoko katika mipango ya vijiji kutokana na uhaba wa muda na fedha ndio maana uchambuzi/mchujo ni muhimu.

**Namna ya kufanikisha utekelezaji**

Ili kufanikisha zoezi la uchambuzi, ni muhimu kutumia vigezo vinavyoendana na hali halisi ya eneo husika na kulingana na kipaumbele cha wilaya. Aidha, vigezo viwiane na sera ya taifa.

**Yanayohitajika**


1. Timu ya Wilaya ya Kuendeleza Mradi (DPDT)
2. Matokeo ya Ukaguzi wa Haraka wa Eneo Husika (takwimu zilizojazwa katika Fomu Na-2)

**Namna qani kazi inafanyika?**

Hatua ndogo ya 1 Fanya matayarisho ya kikao cha uchambuzi.	Washiriki wa kikao ni wajumbe wa DPDT, na DALDO. Watumishi wa Kitengo cha Umwagiliaji cha Kanda na NGO watashiriki kama watazamaji kama wakipatikana.
Hatua ndogo ya 2 Chunguza mtiririko wa mfano wa uchambuzi na urekebishe kama inavyohitajika.	Tazama Mchoro Na-1. Mtiririko unaonyeshwa ni mfano, na unaweza kubadilishwa kulingana na hali ya mahali na kipaumbele cha wilaya. DPDT inabidi kuchunguza kwa makini mfano wa mtiririko wa uchambuzi.
Hatua ndogo ya 3 Chambua skimu za umwagiliaji kama zilivyoainishwa kwenye zoezi la kutembelea eneo na kulingana na mtiririko wa uchambuzi.	DPDT itafanya zoezi la mchujo ili kuanisha skimu zitakazoorodheshwa kwenye DADP. Zoezi hili litafanyika kwa hatua 3: hatua ya kwanza itakuwa ni kuziondoa skimu zisizo na sifa zinazotakiwa, hatua ya pili ni kuzipanga kwa kipaumbele kulingana na ubora, hatua ya tatu ni kuangalia upya kila skimu kwa undani kwa kuzingatia hali halisi ya kila skimu. Ni muhimu kuzingatia chanzo cha maji kwa kila skimu kama ni kutumia pampu, mto wa msimu au mvua.
Hatua ndogo ya 4 Tayarisha taarifa ya ukaguzi wa haraka wa eneo na taarifa ya uchambuzi pamoja na matokeo.	DPDT itaandaa taarifa ya ukaguzi wa haraka wa eneo na taarifa ya uchambuzi kwa kukusanya matokeo ya zoezi la uchambuzi na kuzingatia vigezo vilivyoainishwa. Endapo skimu za umwagiliaji zinazotumia pampu, mito ya msimu na uvunaji wa maji ya mvua zitachaguliwa, basi kwenye taarifa iwekwe wazi sababu za kuchagua skimu hizi. Taarifa pia ionyeshe matatizo yoyote ya kutumia vigezo vilivyotumika ili kuboresha zoezi la uchambuzi likifanyika mara nyingine. <u>Yaliyomo kwenye taarifa ya ukaguzi wa haraka wa eneo na uchambuzi</u> 1. Kipaumbele cha wilaya katika uendelezaji wa umwagiliaji 2. Orodha ya skimu za umwagiliaji katika wilaya (Fomu Na-1 iliyojazwa) 3. Matokeo ya ukaguzi wa haraka wa eneo (Fomu Na-2 iliyojazwa) 4. Vigezo vya uchambuzi na ushindanishi 5. Matokeo ya uchambuzi yakiwa na maelezo ya kina
Hatua ndogo ya 5 Wasilisha taarifa kwenye Kitengo cha Umwagiliaji cha Kanda.	DPDT itawasilisha taarifa iliyotajwa hapo juu kwenye Kitengo cha Umwagiliaji cha Kanda pamoja na karatasi ya upimaji kwa kila skimu kwa ajili ya tathmini na uidhinishaji.

**Kumbuka:** Endapo kuna kazi zinazoendelea hatua kwa hatua, ni vyema kipaumbele kikawa kwa uendelezaji wa kazi hizi.

Mchoro Na-1 Mtiriko wa uchambuzi



Hatua ya 2: Kipaumbele kulingana na Ubora wa Skimu

Mfano wa Vigezo vya Kipaumbele	Alama za Awali	Kigezo cha Wilaya	Alama zilizo-rekebishwa
(1) Tathmini ya Kiufundi			
(a) Vyanzo vya Maji			
Mto wa Kudumu	3		
Mto wa Msimu	2		
Uvunaji wa Maji ya Mvua	1		
(b) Ardhi			
Inafaa kwa kilimo	2		
Dalili za Chumvichumvi	0		
(2) Ari ya Wakulima			
(a) Umoja wa Wamwagiliaji			
Upo na umesajiliwa	3		
Upo lakini haujasajiliwa	2		
Haujaundwa	1		
(b) Uhai wa umoja wa wamwagiliaji			
Hai (vikao, uchaguzi, ukusanyaji wa ada za maji, n.k.)	2		
Sio hai	1		
(3) Matumizi bora ya Mabonde ya Mito			
(a) Hati ya Kumiliki Maji			
Imeshatolewa	2		
Bado haijatolewa	1		
(4) Masoko			
Skimu imeunganishwa na Soko/Wanunuzi	2		
Skimu haijaunganishwa na Soko/Wanunuzi	1		

Hatua-ndogo 1 Chagua vipengele vya mpango wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya DADPs mwaka huu	Chagua shughuli muhimu za kuendeleza mpango wa kilimo cha umwagiliaji katika wilaya kawa ajili ya DADPs kwa mwaka huu. Inapendekezwa kuchukua skimu ambayo imepewa kipaumbele au pamoja na mchanganyiko wa mpango wa ziada wa wilaya. Hata hivyo, kama skimu iliyopewa kipaumbele haijakidhi mahitaji (uhaba wa makubaliano/ mwamko), ni vema mpango wa ziara wa wilaya ukapendekezwa mwaka huu. na uendelezaji wa skimu ukafanyika baadaye.
Hatua-ndogo 2 Toa muhtasari wa mpango wa uandaaji wa skimu	Kamilisha mpango kwa kujaza Fomu Na-15. <ol style="list-style-type: none"> <li>1) Panga mahitaji ya gharama za uendeshaji na matunzo pamoja na gharama za kubadili/kurekebisha kwa ajili ya kuendesha skimu (mchango wa wakulima unaweza ukafikiwiwa)</li> <li>2) Panga mahitaji ya gharama za uanzishwaji wa skimu katika kipindi hiki cha DADPs.</li> <li>3) Kadiria gharama za kuendeleza skimu zitakazo hitajika, ikiwa kuna skimu ambayo imesha pendekezwa kuendelezwa.</li> <li>4) Kadiria gharama za Mpango wa ziada wa Wilaya.</li> <li>5) Toa gharama halisi za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika DADPs.</li> </ol>
Hatua-ndogo 3 Tayarisha taarifa ya mpango wa uandaaji skimu ya umwagiliaji	Tayarisha taarifa ya mpango wa kuandaa skimu ya umwagiliaji ili kuonyesha taratibu zilizo tumika na DPDT katika kufikia maamuzi. Takwimu zote zijazwe katika (Fomu Na-3 hadi Fomu Na-15) ikiambatanishwa na ramani ya mpango wa uendelezaji. Ikiwa skimu zote zitaamuliwa kuwa hazifai kwa kuendelezwa na hakuna skimu iliyopendekezwa katika hatua hii ni vema sababu za maamuzi hayo yaandikwe katika taarifa hii.
Hatua-ndogo 4 Wasilisha taarifa katika Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji	DPDT itawasilisha taarifa katika Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji kwa ajili ya makubaliano ya uhalali

Fomu Na-15 Muhtasari wa Mpango wa Kuanzisha Skimu za Umwagiliaji

Mpango wa kuanzisha skimu ya umwagiliaji kwa ajili DADPs		Katika Mwaka Husika	
Jina la wilaya		Tarehe iliyopangwa	
<b>1) Gharama za uendeshaji na matengenezo pamoja na gharama za kubadilisha</b>			
Orodha ya skimu (tumia karatasi nyingine kama kuna skimu zaidi ya tatu)			
(a)	:	_____	Tsh.
(b)	:	_____	Tsh.
(c)	:	_____	Tsh.
JUMLA	:	_____	Tsh. (I)
<b>2) Gharama za uundaji skimu kwa ajili ya DADP inayofuata</b>			
Gharama zinazohitajika katika uundaji mpango wa skimu kwa matumizi yanayofuata ya DADP		:	_____ Tsh. (II)
<b>3) Mpango wa Uendelezaji wa Skimu</b>			
Jina la skimu _____			
<u>1. Jumla ya gharama za kuendeleza skimu</u> (inapatikana kutoka Fomu Na-13)			
(1) Ujenzi	:	_____	Tsh.
(2) Gharama ndogo ndogo	:	_____	Tsh.
(3) Utawala	:	_____	Tsh.
(4) Uhandisi	:	_____	Tsh.
(5) Uendeshaji na matunzo	:	_____	Tsh.
(6) Gharama za kubadilisha	:	_____	Tsh.
<u>2. Gharama za Mwanzo</u>			
(a) Gharama za mwanzo	:	_____	Tsh. Jumla ya (1) hadi (4) ya 1.
(b) Michango ya wakulima	:	_____	Tsh. Inayokubalika ni 15% of 1-(1) (ujenzi)
(c) Michango wa serikali ya wilaya	:	_____	Tsh. (a) - (b)
<u>3. Mpango wa utekelezaji kwa awamu</u> (uwe umekamilika baada ya Hatua ya 12)			
(kama hakuna mpango wa utekelezaji kwa awamu, ingiza gharama zote za mwanzo katika awamu ya kwanza (c))			
(katika awamu ya-1)			
Awamu-1	:	_____	Tsh. Mwaka wa fedha wa _____
Awamu -2	:	_____	Tsh. Mwaka wa fedha wa _____
Awamu -3	:	_____	Tsh. Mwaka wa fedha wa _____
Awamu -4	:	_____	Tsh. Mwaka wa fedha wa _____
Awamu -5	:	_____	Tsh. Mwaka wa fedha wa _____
JUMLA	:	_____	Tsh. (iwe sawa kama (c) in 2.)
Gharama za kuendeleza skimu kwa mwaka		:	_____ Tsh. (III)
<b>4) Mpango wa Ziada wa Wilaya</b>			
Jina na gharama ya mpango (tumia karatasi nyingine kama kuna skimu zaidi ya tatu)			
(a)	:	_____	Tsh.
(b)	:	_____	Tsh.
(c)	:	_____	Tsh.
JUMLA	:	_____	Tsh. (IV)
5) Gharama za uanzishwaji skimu kwa ajili ya DADPs			Tsh. (jumla ya (I)-(IV))

## Hatua ya 10: Uhalalishaji na Makubaliano na Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda

### Jambo Muhimu

Utekelezaji wa Uhalalishaji na maridhiano uwe wa uwazi na wenye lengo maalum

### Kwanini kazi hii inahitajika?

Kwa kuwa mpango wa uandaaji wa skimu za umwagiliaji ulikuwa umetayarishwa na DPDT, kazi hii inahitaji uwajibikakaji wa wadau wote, kwani mpango uliotayarishwa unahusiana na utekelezaji wa karibu, hivyo ni muhimu kukawepo na uhalalishaji na maridhiano na muhusika wa tatu.

### Namna ya kufanikisha kazi

Timu mahususi iliyoundwa katika hatua ya 4 ipewe jukumu la kupitia taarifa iliyo wasilishwa na DPDT, kuwepo na uwiano kutoka katika hatua ya uchambuzi hadi mpango wa ziada wa wilaya.

### Mahitaji

1. Kamati ya Mapitio ya Kanda (ZRC)
2. Timu ya Wilaya ya Kuendeleza Mradi (DPDT)
3. Taarifa ya mpango wa uanzishwaji wa skimu za umwagiliaji

### Namna qani kazi itafanyika?

Hatua ndogo 1 Taarifa ya mpango wa ya uanzishwaji wa skimu za umwagiliaji.	Mapitio yaelekezwe katika vipengele vifuatavyo: - Matokeo ya upimaji kwa kila skimu - Mpango wa awali wa kila skimu - Taratibu za utoaji kipaumbele - Muhtasari wa skimu - Muhtasari wa mpango wa ziada
Hatua ndogo 2 Tayarisha na wasilisha dodoso la maswali ikiwa kuna sehemu ya taarifa ambayo haikueleweka.	Kamati ya mapitio iwasilishe barua kwa DPDT ikiona kuna sehemu zisizo eleweka, au atembelee eneo husika pamoja na watumishi wa DPDT.
Hatua ndogo 3 Tembelea eneo la skimu	Tembelea eneo la skimu pamoja na watumishi wa DPDT ili kuthibisha hali ya eneo.
Hatua ndogo 4 Tayarisha mapitio ya mpango wa uanzishaji skimu za umwagiliaji.	Kamati ya mapitio itayarishe mapitio ya mpango wa uanzishaji skimu za umwagiliaji baada ya kukusanya matokeo ya mapitio.
Hatua ndogo 5 Kutoa barua ya makubalino na maridhiano kwa DPDT.	Afisa Kanda Umwagiliaji kwa niaba ya ZIU, atawasilisha barua ya "Makubalino na Maridhiano" kwa DPDT, ambayo itaambatanishwa na karatasi za mapitio.



## Hatua ya 11: Warsha ya Mwitiko kwa Skimu Zilizochaguliwa

### Jambo Muhimu

Kutoa mwitiko wa matokeo ya mpango wa kuanzisha kwa wanakijiji kwa skimu zilizochaguliwa

### Kwa nini kazi hii inahitajika?

Kwa kuwa utaratibu wa upimaji wa ardhi uliwashirikisha wanakijiji, hivyo ni muhimu kuandaa warsha kwa lengo la kuwaelimisha wakulima (wananch husika) kuhusu matokeo ya matokeo ya uchambuzi.

### Namna ya kufanya kazi

Maelezo ya kina yatahitajika katika kuwafahamisha wanakijiji umuhimu wa kuchaguliwa skimu yao baada ya kupewa nafasi ya kwanza ya kipaumbele katika DADP, vile vile waeleweshwe sababu ya kutochaguliwa skimu nyingine.

### Mahitaji

1. Timu ya Wilaya ya Kuendeleza Mradi (DPDT)
2. Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya (DALDO)
3. Kamati ya Mapitio ya Kanda (ZRC)
4. Taarifa ya mpango wa kuandaa skimu

### Namna gani kazi itafanyika?

#### (1) Kwa skimu zilizo katika nafasi ya kwanza

Hatua ndogo 1(a)

Wajulishe wanakijiji kuwa skimu yao imechaguliwa baada ya kupewa nafasi ya kwanza katika DADP.

Wafahamishe wakulima kuwa DPDT imetayarisha mpango kufuata taratibu za kitaalamu

DALDO and DPDT wafafanue yafuatayo.

#### 1) Uwezekano wa kutekelezwa

Inapaswa kuwafafanulia kuwa skimu yao bado ni teule chini ya DADP na DPDT, na hivyo isichukuliwe kama ni ahadi ya kuendeleza skimu husika. Ni muhimu wakafahamishwa kuwa utaratibu mzima utachukua muda mrefu kabla ya utekelezaji wake, vile vile utekelezaji unaweza ukaahirishwa kama itabainika kuna matatizo baada ya kufanya tafiti ya ziada. Hata hivyo DPDT wanatakiwa kufafanua zaidi kuwa watajaribu kwa kila hali kuendeleza skimu za umwagiliaji.

#### 2) Mipaka ya eneo litakaloendelezwa

Wanakijiji wafahamishwe kuwa mipaka ya eneo linalofanyiwa uchambuzi (study) linaweza likabadilika baada ya uchambuzi wa kina kutokana na sababu za kitaalamu.

#### 3) Makubaliano ya pamoja katika kijiji (vijiji)

Maelewano kati ya wakulima ndani na nje ya eneo litakaloendelezwa ni muhimu katika uendelezaji wa skimu.

#### 4) Eneo la umwagiliaji wakati wa kiangazi

Wafahamishe wakulima kuwa miundo mbinu ya umwagiliaji huenda isiweze kumwagilia eneo lote wakati wa kiangazi kutokana na uchache wa maji katika chanzo, hivyo utaratibu wa kilimo unaweza ukabadilishwa kutegemea hali iliyopo, kwa mfano kulimo cha kubadilishana/mzunguko kila mwaka.

#### 5) Umuhimu wa kuanzisha taasisi za wakulima siku za baadaye

#### 6) Umuhimu wa kulipa ada ya umwagiliaji baada ya utekelezaji

#### 7) Umuhimu wa kulipa gharama za umwagiliaji baada ya kukamilisha ujenzi

#### (2) Kwa skimu ambazo hazikuchaguliwa katika DADP

Hatua-ndogo 1(b)

Wafahamishe wanakijiji matokeo ya uchambuzi na waelezwe kuwa skimu yao bado iko katika hatua ya kufuatilia.

DALDO na DPDT waeleze yafuatayo.

#### 1) Matokeo ya uchambuzi

Hali halisi ielezwe kwa ufasaha kuwa skimu haikupendekezwa katika DADP mwaka huu.

#### 2) Uwezekano wa kutekeleza baadaye

Wakulima wafahamishwe kuwa bado kuna nafasi ya kupendekezwa katika siku za baadaye, vilevile waeleweshwe sababu iliyopelekea skimu kuto teuliwa kwa kutumia taarifa ya mpango wa kuanzisha skimu.

Kama kuna sehemu inayoweza ikaboreshwa na wanakijiji wenyewe ni muhimu wakafahamishwa ili watiwe moyo na waweze kuongeza juhudi katika shughuli za baadaye.

## Hatua ya 12: Hitimisho la Mpango wa Kuanzisha Skimu ya Umwagiliaji

### Jambo Muhimu

Kupitia upya na kukamilisha mpango wa kuanzisha skimu ya umwagiliaji kama ilivyoshauri DASAC

### Kwa nini kazi inahitajika

Kuna sekta nyingi katika kilimo, lakini uendelezaji wa skimu kutoka sekta ndogo hauingizwi katika DADPS kutokana na ufynywa wa fedha zinazotengwa. Hivyo, ni muhimu kwa mipango ya kuanzisha skimu za umwagiliaji iliyoandaliwa iwasilishwe kwenye Kamati ya Ushauri wa Kilimo ya Wilaya (DASAC) kama moja ya mpango wa maendeleo kutoka sekta ndogo ya kilimo cha umwagiliaji. Ni muhimu kufikiria utaratibu wa kutekeleza kwa awamu kama fedha zitakazotengwa hazitoshi kuendeleza eneo lote kwa wakati mmoja.

### Namna ya kufanikisha kazi

Mpango wa kuanzisha skimu ya umwagiliaji uliotayarishwa uwakilishwe kwa DASAC ukiwa kamili ili waweze kuelewa.

### Mahitaji

1. Timu ya Wilaya ya Kuendeleza Mradi (DPDT)
2. Muhtasari wa skimu pamoja Muhtasari wa Mpango wa Ziada wa Wilaya
3. Kamati ya Ushauri wa Kilimo ya Wilaya (DASAC)

### Namna qani kazi inafanyika?

Hatua ndogo 1 Wasilisha mpango ulitayarishwa kwa DASAC	Wasilisha Fomu Na-13 hadi 15 kwa DASAC kwa ajili ya tathmini
Hatua ndogo 2 Tia maanani utekelezaji wa mpango kwa awamu	Ni muhimu kufikiria kufanya uendelezaji kwa awamu kama DASAC itaomba kupunguza gharama za uendelezaji kwa mwaka huu. Suala la gharama za uendeshaji na matunzo katika skimu zilizopo lipewe kipaumbele, likifuatiwa na mpango wa kuendeleza skimu au mpango wa ziada wa wilaya baada ya kupata maoni kutoka DASAC. Pitia Fomu Na-15. <u>Uendelezaji kwa awamu</u> Kama sehemu inayokusudiwa kuendelezwa inatarajiwa kuwa na mafuriko, ni vema tuta la kukinga mafuriko likajengwa kabla ya ujenzi kuanza ili kuzuia uharibifu wa miundombinu inayokusudiwa kujengwa.
Hatua ndogo 3 Wasilisha mpango wa mwisho kwa DASAC na ZIU	Wasilisha Fomu Na-13 hadi 15 kwa DASAC na ofisi ya Umwagiliaji Kanda. Ofisi ya Kanda inatakiwa kuwasilisha kwa DITS kitengo cha Takwimu.

### Sandukuu

#### Uendelezaji kwa Awamu

Katika kuandaa mpango wa kuendeleza skimu za umwagiliaji, ni muhimu kuangalia kiasi cha kazi kitakachohitajika, muda na fedha iliyotengwa kwa shughuli hiyo.

Ikiwa kazi hiyo haitamalizika katika kipindi cha mwaka mmoja wa fedha, ni vema utekelezaji wake uwe wa awamu.

Mfano:

- (1) Tenganisha awamu ya uchambuzi/usanifu na utekelezaji
- (2) Wakati wa utekelezaji, fikiria mfereji mikubwa na ile ya matoleo

## Sehemu ya 4

*Mchakato wa kuendeleza umwagiliaji  
baada ya hatua ya DADP*



## Sehemu ya 4 Mchakato wa kuendeleza umwagiliaji baada ya hatua ya DADP

### (1) Utangulizi/Jumla

Skimu za umwagiliaji katika DADPs zitaendelezwa zikizingatia mwongozo wa Uboreshaji Shirikishi kwenye Miradi Iliyoanzishwa na Kusimamiwa na Wakulima Wadogo Wadogo, Julai 2003. Katika mwongozo huo ambao yaliyomo yameelezwa kifupi katika sehemu ya (4) ya utangulizi, njia inayopendekezwa kuendeleza skimu za umwagiliaji baada ya uchaguzi wa shughuli za skimu inaainishwa kama ifuatavyo (rejea mwongozo uliotolewa kwa kina).


### (2) Njia ya kuendeleza skimu za umwagiliaji baada ya uchaguzi

Baada ya uchambuzi wa skimu kwa ajili ya DADPs, skimu zilizochambuliwa zitaendelezwa katika dhana shirikishi. Njia hii ina hatua tisa zifuatazo:

- 1 Mpango wa kazi shirikishi
- 2 Usajili wa kisheria/Hati ya maridhiano
- 3 Upembuzi wa ugunduzi shirikishi
- 4 Usanifu shirikishi/Upembuzi yakinifu
- 5 Uamuzi wa uwekezaji wa pamoja/Makubaliano ya malipo
- 6 Usanifu wa kina/Nyaraka za zabuni
- 7 Tangazo la zabuni/Mkataba
- 8 Utekelezaji
- 9 Uendeshaji na utunzaji

Wadau (wamwagiliaji), kama wahusika wakuu kwa sehemu kubwa katika hatua hizi. Wakala wa serikali wanaohusika katika kila hatua wameonyeshwa katika jedwali la kulia

#### Jinsi ya kuendeleza skimu ya umwagiliaji



Shughuli zilizotajwa katika miongozo:

**Shughuli Kuu katika kila hatua**

Hatua	Shughuli kuu
1 Mpango wa kazi shirikishi	Milolongo ya warsha za mipango ya muda mfupi , - kubainisha hali ya kuhusika kwa wamwagiliaji - kueleza wajibu wa utengaji wa gharama za shughuli za maandalizi
2 Usajili wa kisheria/Hati ya maridhiano	- Kuandikisha/kusajili skimu kama umoja/ushirika/kampuni itavyopendekezwa na wanachama chini ya kanuni/taratibu zilizopo. - Maandalizi na uwekaji sahihi wa LoU kutoka kwenye mradi hadi Halmashauri ya Wilaya
3 Upembuzi wa ugunduzi shirikishi	- Uchambuzi shirikishi wa fursa na vikwazo, uundaji wa miti ya matatizo na matumaini. - kukusanya takwimu za msingi
4 Usanifu shirikishi/Upembuzi yakinifu	- Uchunguzi wa pamoja kati ya wajumbe wa mradi, wadau wengine na wataalamu - kukabidhi matokeo kwa umoja wa wamwagiliaji kwa uidhinisho
5 Uamuzi wa uwekezaji wa pamoja/Makubaliano ya malipo	- Kupokea na kukubali taarifa sahihi ya upembuzi wa watoa fedha. Watoa fedha /wafadhili kupokea & kukubaki taarifa sahihi ya upembuzi - Maandalizi na kusaini mikataba/makubaliano
6 Tangazo la zabuni/Mkataba	- Uchunguzi na usanifu yakinifu wa miradi midogo
7 Utoaji tenda/mkataba	- Kuchambua na kuajiri washauri nasaha kutokana na kikao cha Halmashauri ya Wilaya - Ununuzi wa bidhaa na kuanza kazi kwa mujibu na taratibu za Halmashauri ya Wilaya
8 Utekelezaji	- Jitihada za pamoja kati ya wahusika mbalimbali, hasa wakiwemo wamwagiliaji
9 Uendeshaji na utunzaji	- Kueleza kupitia stadi za uchunguzi shirikishi na upembuzi yakinifu

*Chanzo: Miongozo ya uboreshaji shirikishi kwa miradi ya umwagiliaji iliyoanzishwa na kusimamiwa na wakulima wadogo Julai 2003*

Ili kukidhi utekelezaji wa shughuli hizi kikamilifu, ni lazima ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda kusaidia wataalamu wa Wilaya kwa kufanya nao mawasiliano ya karibu.

**(3) Uongozi wenye kuhiari mchakato ya maendeleo**

Miongozo huonyesha ratiba ya maendeleo/ukuaji. Kulingana na ratiba, miaka miwili ingehitajika kwa uchunguzi, kusanifu na ununuzi wa vifaa kabla ya utekelezaji. Kwa upande mwingine hatua za maendeleo ya skimu/miradi ya umwagiliaji hugubika/hujumuisha tofauti mbalimbali za ukubwa, kwa mfano hekta 10 hadi 500 ni kwa miradi midogo ya umwagiliaji. Kwa nyongeza, kila mradi wa umwagiliaji una hatua tofauti ya ukamilikaji. Kwa maana hii, baadhi ya hatua zilizotajwa hapo juu zingeweza kurukwa /kuachwa au kufupishwa muda kutegemea na hali ya skimu. Usimamizi/uongozi wenye kuhiari unatakiwa.



## Sehemu ya 5

*Matumizi ya takwimu*

*katika kuandaa skimu za umwagiliaji*



---

## Sehemu ya 5 Matumizi ya takwimu katika kuandaa skimu za umwagiliaji

### (1) Utangulizi

Katika Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi ya Wizara ya Kilimo na Chakula, mfumo rahisi wa utunzaji takwimu umeanzishwa kwa lengo la ushirikianaji wa takwimu na taarifa na Halmashauri ya Wilaya, na pia kuweza fahamu juu ya maendeleo ya umwagiliaji yanayotekelezwa na serikali hizo. Mfumo wa takwimu zilizoandaliwa utakuwa na sehemu mbili. Takwimu zilizoandaliwa za Umwagiliaji, na Mfumo wa taarifa wa kijiografia wa umwagiliaji. Halmashauri ya Wilaya inaweza kuwasiliana na kitengo hiki (*database*) wakati wowote inapotakiwa. Katika sehemu hii mnyumbulisho wa mfumo wa kuhifadhi takwimu unaelezwa

### (2) Takwimu muhimu zipatikane kutoka mfumo wa takwimu zilizohifadhiwa

Taarifa muhimu zifuatazo hupatikana katika mfumo wa takwimu zilizohifadhiwa. Inashauriwa ni vema taarifa hizi zipatikane kabla ya kuanza kupanga maendeleo ya umwagiliaji.

#### Taarifa muhimu inayotunzwa katika *database* za umwagiliaji

- Matokeo ya orodha ya miradi ya umwagiliaji yaliyofanywa 2002
- Vipimo vya ramani 1:250,000 na 1:50,000 (Ramani zimeandaliwa na kuingizwa kwenye hifadhi ya kompyuta, hivyo watumiaji wake wanatahadhirishwa kuthibitisha vipimo vya ramani hizo watakapohitaji kuzitumia. Utengenezaji wa takwimu haujakamilika, kwani baadhi ya ramani za awali hazipo. Angalia Jedwali Na-5)
- Vigezo vya usanifu na nyaraka rejea kuhusiana na umwagiliaji

#### Taarifa muhimu inayotuzwa katika mfumo wa taarifa ya kijiografia (GIS) wa umwagiliaji

- Ramani ya mvua
- Ramani ya sura ya nchi (uoto)
- Ramani ya mgawanyo wa ardhi
- Ramani ya aina za udongo
- Ramani ya mahusiano ya kilimo
- Ramani ya maeneo yaliyohifadhiwa

### (3) Taarifa ya uwasilishaji wa matokeo ya kuandaa mpango kwenye kitengo cha takwimu

Inapendekezwa kwa msisitizo kupeleka matokeo ya uundaji wa skimu za umwagiliaji katika kitengo cha takwimu, kwani moja ya majukumu muhimu ya Wizara ya Kilimo na Chakula ni mipangilio ya skimu za umwagiliaji maji za nchi nzima.


(4) Mfumo wa utunzaji takwimu

Hadi sasa (2004) takwimu zilizohifadhiwa kwenye mfumo wa takwimu (*database*) ulioko kilimo III, bado haujawa tayari kwa usambazaji kupitia tovuti. Kwa hiyo Halmashauri na Wilaya na Wadau wengine wanaombwa kuwasiliana na kitengo cha usimamizi wa takwimu na taarifa cha Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kutumia fax na/au simu. Huduma za posta pia zinaweza kutumika katika ushirikianaji wa takwimu na taarifa.

**Sanduku**


***Kitengo cha Usimamizi wa Takwimu na Taarifa***

*Wahusika wakuu ni: Mhandisi January Kayumbe and Mr. Amandus Lwena*  
*Simu/Fax No.:022-2865426*  
*Anwani: Idara ya umwagiliaji na Huduma za Ufundi Kilimo III, Temeke, SLP*  
*9192, Dar es Salaam*



Jedwali Na-5 Kielelezo cha ramani za topografia

## *Viambatanisho*



## **Kiambatanisho-1**

*Miongozo na Taratibu Muhimu*

## Miongozo na Taratibu Muhimu

### 1. Mwongozo wa mpango wa maendeleo ya kilimo katika wilaya DADPs

DADP ni mpango endelevu wa miaka 3 wa kuendeleza sekta ya kilimo katika ngazi ya Wilaya na Kijiji chini ya programu ndogo, kama ilivyo ainishwa katika Sekta ya Maendeleo ya Kilimo (ASDP). Mwongozo wa kuandaa DADPs ulitolewa Januari 2003 na kusahihishwa Novemba 2003. Katika masahihisho hayo, Halmashauri ya Wilaya kama kiungo inatakiwa kutekekeleza majukumu 3 yafuatayo: (i) Kutafsiri sera ya Taifa na mwongozo wa bajeti kulingana na hali halisi ya Wilaya (ii) Kuandaa matarajio ya Wilaya kwa kuanisha matarajio toka nje na ndani (iii) Kuchagua mipango ya miradi iliyoandaliwa na wanavijiji. Ufuatao ni ufafanuzi kwa hatua katika kuandaa DADPs.

#### Hatua za kuandaa DADP

Hatua	Shughuli	Muhusika	Muda
0	Kutoa maelekezo na kuandaa mfumo wa habari.	ASLMS, PO-RALG na Secretarieti ya ASDP	October
1	Kuelewa mfumo wa upangaji	DALDO	October
2	Kuandaa Warsha ya uzinduzi	DALDO	October- November
3	Kuunda timu ya mpango	DALDO	October- November
4	Uchambuzi wa hali ya Wilaya na kuweka mwelekeo.	DASAC	November
5	Kuandaa mipango ya Kijiji	DPDT na wanakijiji	December- January
6	Kupitisha mipango ya kijiji	Mkutano mkuu wa kijiji, WDC+DASAC	January- February
7	Usimamizi shirikishi na tathmini ya mpango	DASAC	February
8	Kuwasilisha DADPs	RCC, Halmashauri ya wilaya, & DASAC	Mwisho wa FEB- APR Mwanzoni

*Chanzo: Mwongozo kwa ajili ya mpango wa maendeleo ya kilimo ya wilaya, November 2003*


*Angalizo: ASLMS (Wizara zinazoongoza katika sekta ya ya kilimo: KC, UM na WMM)*

*PO-RALG (Ofisi ya raisi tawala ya mkoa),*

*DALDO (Afisa kilimo/mifugo wa wilaya), WDC (Kamati ya maendeleo ya Kata) DASAC (Kamati ya ushauri katika sekta ya kilimo), RCC (kamati ya ushauri ya mkoa)*

Jedwali lifutalao linatoa maelekezo jinsi ya kuandaa DADPs hatua kwa hatua.

Utaratibu wa Kutayarisha Mpango wa DADPs kwa Hatua



Kwa nyongeza, mwongozo unaelezea njia ya mpango shirikishi kama ilivyo elekezwa kutumika rasmi na Serikali Kuu ili kupata mipango ya miradi toka vijijini. Njia hii huitwa Fursa na Vikwazo katika Maendeleo (O&OD) na utaratibu wake wa utekelezaji ni kama ufuatavyo:

Njia ya mpango shirikishi (fursa na vikwazo vya maendeleo)

Na	Shughuli
1	Kuzindua mkutano mkuu wa kijiji
2	Kukusanya takwimu kitaalamu - Ramani ya kijiji: inayoonyesha rasilimali ya jamii, vitu vilivyomo na mipaka. - Matembezi ya mshikamano: kuhakiki taarifa iliyokusanywa katika ramani ya kijiji ikibainisha fursa na vikwazo katika mwaka mzima.
3	Kukusanya takwimu za nyakati tofauti zilizopita - Matukio ya kihistoria: orodhesha matukio na juhudi zilizofanyika, hii itasaidia kuboresha mipango ya baadaye kwa matukio yanayofanana - Takwimu za nyakati/msimu: kuonyesha sehemu kubwa ya taarifa mbalimbali za nyakati ikiwa ni kwa vipindi vya fursa na vikwazo kwa mwaka
4	Kukusanya takwimu za kijamii - Mahojiano ya vikundi: huboresha vikundi mbalimbali kama vile wanawake, wanaume vijana na vikundi vilivyoathirika pamoja na kuendeleza mipango ya kijiji - Shughuli zinazotekelezwa kila siku kijinsia: hutoa taarifa ya mgawanyo wa kazi kiumri na kijinsia. - Ramani ya rasilimali kijinsia: kueleza nani anamiliki, nani anadhibiti, nani anatoa nguvu kazi na uwajibikaji juu ya rasilimali zilizopo kijinsia
5	Kuandaa mpango wa kijiji Chukua takwimu za ziada toka kijijini na taasisi nyingine zilizopo kijijini kanma shule za msingi na zahanati.
6	Kupitisha mpango wa kijiji katika mkutano mkuu wa kijiji

Chanzo. Mwongozo wa DADPs, Novemba 2003

Mwongozo kwa ajili ya kuandaa miradi ya umwagiliaji katika wilaya, utatumika kulingana na mfumo wa mwongozo wa kutayarisha DADPs.

## 2. Mwongozo na taratibu katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji

Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula imetoa miongozo na taratibu mbali mbali kupitia miradi yake katika kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji nchini nayo ni kama ifuatavyo:

- Mwongozo shirikishi katika uboreshaji wa miradi midogomidogo ya umwagiliaji maji iliyoanzishwa na kusimamiwa na wakulima, Julai 2003
- Mwongozo wa kupanga miradi ya umwagiliaji (angalia kiambatisho 1)
- Mwongozo wa kusanifu miradi ya umwagiliaji (angalia kiambatisho 1)
- Mwongozo wa kusanifu miradi ya uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yenye ukame (angalia kiambatisho 1)
- Mwongozo wa matumizi bora ya maji ya umwagiliaji kwa wataalamu wa ugani (angalia kiambatisho 1)

Yafuatayo ni maelezo ya mwongozo na taratibu zilizotajwa hapo juu kwa ajili ya kumbu kumbu kwa watumishi wa wilaya.

### (1) Mwongozo Shirikishi katika Uboreshaji wa Miradi Midogomidogo ya Umwagiliaji Iliyoanzishwa na Kusimamiwa na Wakulima, Julai 2003

Mwongozo huu ulitayarishwa ili utumike kwa ajili ya programu zote za umwagiliaji katika ngazi ya taifa, mkoa na wilaya Katika uboreshaji wa aina zote wa miradi midogo ya umwagiliaji iliyoanzishwa na kusimamiwa na wakulima wadogo kama ilivyopendekezwa kisekta katika programu ya ASDP. Mbali na kuwa mwongozo huu ulitayarishwa kwa ajili ya ukarabati na /au uboreshaji wa skimu zilizopo, vile vile kimsingi unaweza ukatumiwa kwa ajili ya kuendeleza miradi mipya. Utekelezaji wa Mwongozo huu unafuata mfumo wa hatua kwa hatua ya mpango shirikishi katika uendelezaji wa miradi midogomidogo yenye gharama nafuu na faida iliyoanzishwa na kusimamiwa na wakulima wadogowadogo. Hatua kumi na moja zinazotumika ni kama ifuatavyo:

Mfumo wa Hatua kwa Hatua

Na	Shughuli
0	Uchaguzi wa Wilaya
1	Uchaguzi wa miradi/skimu
2	Kuandaa Mpango kazi shirikishi
3	Uandikishaji wa uhalali/ruhusa ya kuanza
4	Uchaguzi wa ugunduzi shirikishi
5	Usanifu shirikishi/upembuzi yakinifu
6	Uamuzi wa uwekezaji wa pamoja/maelewano ya malipo
7	Usanifu wa kina/nyaraka za zabuni
8	Kutoa zabuni/mikataba
9	Utekelezaji
10	Uendeshaji & matengenezo

*Chanzo. Miongozo kwa uboreshaji shirikishi kwa miradi midogo ya umwagiliaji iliyoanzishwa na kusimamiwa na wakulima wadogo*

Kama inavyoonekana katika jedwali; mwongozo hauonyeshi jinsi ya kuchagua miradi ya umwagiliaji kutoka kwa wakulima kupitia kwenye Halmashauri ya Kijiji. Miradi yote ya umwagiliaji inadhaniwa kuwa katika mikono/usimamizi wa ofisi ya wilaya, ingawa uchaguzi wa Wilaya hutajwa kwa dhana ya wafadhili kusaidia programu.



Katika kila hatua ya maendeleo ya mradi chini ya DADP, mwongozo unaeleza wazi “kwa nini” “vipi” “nani” na “matokeo”. Mfumo huu huwezesha wataalamu wa wilaya wanaohusika kuelewa taratibu zinazotumika katika maendeleo, hivyo mwongozo huu ni wa manufaa kwao.

## (2) Mwongozo wa Kupanga Kuandaa Miradi ya Umwagiliaji

Mwongozo huu una sehemu 11 kama ifuatavyo:

Yaliyomo katika mwongozo

sehemu	Kichwa cha habari
1	Upembuzi wa awali wa miradi ya umwagiliaji iliyopendekezwa
2	Upimaji wa sura ya eneo
3	Upimaji wa ardhi na kubainisha matabaka ya ardhi
4	Hali ya hewa na maji
5	Kuchambua hali ya kiuchumi na kijamii
6	Kilimo (Agronomia)
7	Mahitaji ya maji ya umwagiliaji
8	Uhandisi
9	Uongozi, Uendeshaji na Utunzaji
10	Uchambuzi wa mipango ya fedha na uchumi
11	Taarifa ya upembuzi

Mwongozo huu umeandaliwa ili kutoa kanuni au taratibu zitakazo fuatwa katika uchunguzi na tafiti ambazo zitahitaji upembuzi yakinifu. Mwongozo unahusisha/jumuisha vipengele vyote muhimu kwa kuandaa mradi wa umwagiliaji kuanzia upimaji hadi tathimini, ingawa mpango wa uvunaji maji haukujumuishwa. Kutokana na taratibu zilizotajwa, mwongozo huu unaelekea zaidi kulenga miradi ya kati hadi mikubwa, ambayo huitwa ya kisasa katika Tanzania.

Kama ilivyobainishwa katika mwongozo, watumiaji wake wengi wanatarajiwa kuwa wataalamu wa kupanga miradi wa kitengo cha Umwagiliaji Kanda na I dara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Kwa hali hiyo, mwongozo huu huenda usiwe na manufaa kwa watu wasio na ufahamu wa kutosha, ingawa ni mwongozo mzuri kwa watu wenye uelewa wa kati wanaotaka kujifunza zaidi.

## (3) Mwongozo wa Kusanifu Miradi ya Umwagiliaji

Mwongozo huu una sehemu mbili ambazo ni : Taratibu/ Kanuni na michoro. Mwongozo una jumla ya sura 10 kama zifuatavyo:

Yaliyomo katika Mwongozo

Sura	Kichwa cha habari
1	Taratibu/kanuni za kutambua mradi
2	Uchunguzi wa eneo na upimaji
3	Uchunguzi wa vyanzo vya maji
4	Mahitaji ya maji
5	Utoaji wa maji shambani
6	Usanifu wa mradi wa umwagiliaji
7	Usanifu wa miundombinu
8	Usanifu wa banio
9	Usanifu wa vichuja mchanga
10	Kuandaa michoro ofisini katika kiwango kinachotakiwa

Mwongozo hutoa shughuli zilizo muhimu kwa ajili ya kusanifu kwa kina. Mwongozo unaweza kuwa wa manufaa kwa wataalamu wa serikali wenye uzoefu katika kusanifu miradi ya umwagiliaji, lakini ina usumbufu kwa wenye uzoefu mdogo kama wataalamu wa wilayani, kwa sababu miongozo iliandaliwa kwa kurejea maandiko ya kiufundi yaliyomo katika vitabu vya FAO juu ya Umwagiliaji na Utoaji maji mashambani. Kwa nyongeza, miongozo haihusiki na njia ya usanifu shirikishi kama swala muhimu kwa sasa.

**(4) Mwongozo wa Kusanifu Miradi ya Umwagiliaji kwa Njia ya Uvunaji Maji ya Mvua katika Maeneo yenye Ukame**

Mwongozo huu umeandaliwa katika Programu Shirikishi ya Maendeleo ya Kilimo cha Umwagiliaji (PIDP) ikilenga usanifu wa uvunaji wa maji ya mvua, ambao umepewa kipaumbele katika maeneo yenye ukame. I na shughuli kumi na moja kana ifuatavyo:

**Yaliyomo katika miongozo**

Sura	Kichwa cha habari
1	Mchakato wa mbinu na njia ya utambuzi
2	Uchunguzi wa eneo na upimaji
3	Uchunguzi wa vyanzo vya maji
4	Mahitaji ya maji ya mradi
5	Malambo na matuta ya udongo
6	Utoaji wa maji shambani
7	Kusanifu mradi wa umwagiliaji
8	Kusanifu miundombinu ya umwagiliaji
9	Kusanifu vigawa maji.
10	Kusanifu vichuja mchanga
11	Makisio ya gharama za mradi

Kati ya sura 11, baadhi yake ni ngeni na nyingine ni marudio kutoka katika Mwongozo wa Kusanifu Miradi ya Umwagiliaji zilizotajwa hapo awali.

**(5) Mwongozo wa Matumizi Bora ya Maji katika Kilimo cha Umwagiliaji kwa Maafisa Ugani**

Mwongozo huu umeandaliwa kwa msaada wa Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (ASPS), ambao umelenga kuwapatia maafisa ugani waliopo vijijini elimu inayohusu matumizi bora ya maji pamoja na kuwajengea uwezo. Mwongozo huu una sura kumi zifuatazo:

**Yaliyomo Kitabuni**

Sura	Kichwa cha habari
1	Utangulizi
2	Chanzo cha maji
3	Upimaji wa maji ya umwagiliaji
4	Mifumo ya umwagiliaji na njia za kusambaza maji mashambani
5	Mahusiano ya kimsingi kati ya ardhi-maji -mmea
6	Mahitaji ya maji kwa mmea
7	Uendeshaji wa miundo mbinu ya umwagiliaji.
8	Utoaji maji mashambani
9	Kutengeneza, na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji
10	Muundo wa kikundi cha umwagiliaji
11	Masuala ya mazingira katika mifumo ya umwagiliaji

Mwongozo umeandaliwa ili kuwezesha wataalamu wa ugani kuelewa kirahisi usimamizi wa maji pamoja na uundaji, uandikishaji na uendeshaji wa kikundi cha umwagiliaji. Aidha,

mwongozo unajumuisha athari za mazingira yanayoletwa na maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji kama (i) kupungua ubora wa ardhi (ii) kupungua ubora wa maji ya chini ya ardhi(iii) kupungua ubora wa maji yaliyo juu ya ardhi (iv) kutuama kwa maji. Njia na taratibu za kupunguza au kurekebisha athari hizi pia zimebainishwa. Kwa ujumla mwongozo unatoa elimu ya kutosha ya rejea kwa watumishi waliopo wilayani katika fani nyingine za kilimo pamoja na maafisa ugani.

## *Kiambatanisho-2*

*Muhtasari wa Mpango Kabambe  
wa Taifa wa Umwagiliaji*

## Muhtasari wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji

[Hali ya nyuma]

Mpango wa taifa wa maendeleo ya umwagiliaji (NIDP) ulioandaliwa 1994 unahitaji kusahihishwa kutokana na utekelezaji wake usiotosheleza mahitaji ya sasa. Aidha hauendani na sera na mikakati ya serikali kama ile ya mwongozo/mipango ya kilimo na mifugo wa "1997." Dira ya maendeleo ya Tanzania 2005, 2000, na mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo 2001. Serikali ya Tanzania iliomba Serikali ya Japan kurefusha kipindi cha misaada yake ya kiufundi na kufanya uchunguzi juu ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (NIMP). Serikali ya Japan ilikubali ombi hilo, na mkataba wa kazi ukasainiwa na pande zote mbili mnamo April 10, 2001.

[Malengo]

- Kuandaa mpango Kabambe wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji katika ngazi ya taifa ifikapo mwaka 2017
- Kuwaelimisha kwa kutoa mafunzo kwa watalaamu wa Tanzania wawapo kazini katika kipindi chote cha zoezi hili

[Jinsi ya kufanya upembuzi]


Hakuna shaka kuwa kilimo cha umwagiliaji kinachangia katika kusaidia kuimarisha uzalishaji wa mazao. Hata hivyo, umwagiliaji peke yake hauwezi kuonyesha ongezeko la mazao ya kilimo bila kushirikisha sekta nyingine ndogo kama pembejeo za kilimo na huduma za ushauri wa ugani. Hivyo sekta hizo ndogo zinahitaji kuendelezwa kwa karibu pamoja na umwagiliaji, ili ziweze kutoa mafaniko yanayotarajiwa.

Mkakati wa kitaifa wa kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDS) unaeleza kuwa lengo lake la msingi ni kujenga hali nzuri inayowezekana ya mazingira ili kuboresha uzalishaji wenye faida wa sekta ya kilimo kama msingi wa kuboresha mapato ya kilimo na kupunguza umaskini kwa vipindi vya muda wa kati hadi mrefu. Kwa kuzingatia mikakati iliyoenezwa katika ASDS na falsafa ilyotolewa na NIDP pamoja na matokeo ya upembuzi, "Maendeleo Endelevu ya Umwagiliaji" ilipendekezwa kwamba kusudi la NIMP liwe ni umuhimu wa "utumiaji kikamilifu wa rasilimli za taifa". Hakika hii itachangia katika kufikia lengo la msingi la ASDS.

*"Mandeleo endelevu ya umwagiliaji"* humaanisha uanzishaji wa miradi ya umwagiliaji inayojitegemea kiufundi na kifedha pamoja na kuimarika kwa taasisi na uongozi wake.

Upembuzi wa kwanza ulifanyika ili kuainisha matatizo ya miradi ya umwagiliaji iliyopo na kubaini fursa za umwagiliaji. Kutokana na matokeo haya, dhima ya maendeleo ya hatua kwa hatua ilipendekezwa na kuwa ya miaka 15 kutoka 2003 hadi 2017 katika mpango mzuri wa sera, uchumi wa taifa na kisio la mahitaji ya chakula kikuu. NIMP ulitayarishwa kwa kufuata utaratibu wa utoaji mafunzo pmoja na kuwa na mshikamano wa karibu kati yao, kama mkakati wa kuleta maendeleo endelevu wa umwagiliaji. Ufuatao ni mtiririko wa uandaaji wa NIMP.

## Utaratibu wa kutayarisha Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji



Pointi muhimu za stadi,

[Upembuzi wa tatizo]

Katika upembuzi, uainishaji wa tatizo ulifanyika kutokana na matokeo ya warsha ya PCM na upimaji wa kuhakiki skimu 1,428 za umwagiliaji zilizopo na zilizo pendekezwa na pia ukusanyaji wa takwimu toka wakala mbali mbali.

«Warsha za PCM»

Masomo na wahusika na washa husika, yameonyeshwa katika jedwali la kulia.

Katika mafunzo, washa ya PCM ilifanyika mara 5 na uainishaji wa lengo ulifanyika kwa uainishaji wa tatizo kwa kila somo.

«Upimaji wa kuhakiki»

chambuzi ulifanyika kwa skimu 1428, kati ya hizi skimu 739 zilihakikiwa na mradi wa umwagiliaji uliofadhiliwa na benki ya dunia, na 689 zilihakikiwa na NIMP kama matokeo ya upembuzi katika Tanzania bara. Uhakiki huo ulibainisha kuwa eneo lote la umwagiliaji ni hekta 854,000.

[Kukadiria maeneo yanayofaa Kwa umwagiliaji]

Kwa jumla, ufaaji wa maeneo ya umwagiliaji hukadiriwa kutokana na rasilimali ya maji iliyopo na rasilimali za ardhi ifaayo. Katika upembuzi huu, rasilimali za uchumi wa kijamii pia zilifikiriwa, kwani hali ya soko pia ni muhimu kwa maendeleo ya umwagiliaji na kwa kiasi kikubwa uchangia katika uchaguzi wa miradi ya umwagiliaji. Eneo linaloweza kuendelezwa katika umwagiliaji, lilipatikana baada ya mapitio ya ramani za ukaguzi na kuzibebesha moja juu ya nyingine, na baadaye maeneo ya miradi ya umwagiliaji yaliyohakikiwa na kuingizwa katika ramani inayoonyesha maeneo yanayofaa. Matokeo

Masomo	Washiriki
Ufahamu juu ya uendeshaji wa umwagiliaji	Kitengo cha umwagiliaji cha (Wizara ya kilimo na chakula) ofisi ya umwagiliaji kanda
Utendaji usioridhisha wa kitengo cha umwagiliaji.	Kitengo cha umwagiliaji cha MAFS Ofisi ya Umwagiliaji kanda Meneja wa miradi ya umwagiliaji
Msaada hafifu wa kilimo cha umwagiliaji toka serikali za mitaa	Halmashauri ya wilaya , Maafisa ugani
Uhaba wa maji katika ploti za mashamba	Vikundi vya umwagiliaji Maafisa ugani
Maendeleo hafifu ya kilimo cha umwagiliaji	Wawakilishi wa wakulima Halmashauri ya wilaya

yalitumiwa katika kuandaa mpango wa maendeleo wa mkoa.

Viashiria vilivyotumiwa katika upenguzi ni kama ifuatavyo:-

«Rasilimali za Ardhi»

Rasilimali za ardhi zilitathminiwa kwa kutumia ramani ya uoto wa ardhi, ramani ya sura ya eneo, na ramani inayoonyesha sehemu ya ardhi kama inavyo onekana katika jedwali la kulia:

«Ramani za maji»

Sehemu zenye maji ya kutosha ni zile zenye mtiririko unaozidi  $1.0m^3/sec/500km^2$ .


«Rasilimali za uchumi kijamii»

Rasilimali za uchumi kijamii zilichunguzwa kwa kutumia viashiria vitatu yaani msongamano wa watu, wingi wa barabara na uzalishaji wa chakula kama inavyoonyeshwa katika jedwali la kulia:

[Uchunguzi mbadala wa mpango wa maendeleo]

Kupitia uchambuzi wa matumizi halisi ya maendeleo na matumizi ya kila siku kwa maendeleo ya umwagiliaji kutoka mwaka 1998/1999 hadi 2002/2003,

fedha iliyokuwa inategemewa kutolewa ililenga katika viwango vitatu kama ifuatavyo; kiwango cha juu, kiwango cha msingi na kiwango cha chini. Ulinganishaji wa makadirio ya mahitaji ya mpunga katika vipengele vyote vitatu ilionyesha kuwa kuendeleza umwagiliaji katika kiwango cha juu ungetosheleza mahitaji ya mpunga kufikia mwaka 2017 ikiwa matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo yatatiliwa maanani. Hivyo mwelekeo wa maendeleo katika NI MP ulilenga matumizi ya kiwango cha juu.



Mahitaji ya uchambuzi wa kina

	Kiwango cha msingi (Base case)	Kiwango cha juu (High case)	Kiwango cha chini (Low case)
Kiwango cha ukuaji GDP	5.8% kwa 2003/4 - 007/08 5.9% kwa 2008/9 - 012/13 6.0% kwa 2013/14 - 2017/18	1.0% kwa mwaka juu ya kiwango cha msingi	5.1% kwa mwaka kwa muda wote wa NI MP
Bajeti ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji	1.5%	1.7%	1.5% (hakuna mabadiliko)
Bajeti nje ya bajeti ya serikali (Msaada wa Wafadhili)	100% (Sehemu ya fedha kutoka nje)	110%	100% (hakuna mabadiliko)
Kiasi cha fedha (Shilingi za Tanzania katika mamilioni)	350,042	451,251	327,967
Kiasi cha fedha (Dola za Marekani katika mamilioni)	369	475	345

**【Mwelekeo wa maendeleo wa hatua kwa hatua】**

Programu ya maendeleo ya kutekeleza NIMP inalenga kuanzisha mfumo endelevu wa umwagiliaji ifikapo 2017 katika mwelekeo wa maendeleo wa hatua kwa hatua.: Muda mfupi (2003 - 2007), Muda wa kati (2003 - 2012), na Muda mrefu (2003 - 2017), kama ilivyotajwa hapo juu. NIMP ilipendekeza hatua mbili za utekelezaji ambazo ni utoaji wa mafunzo na kuendeleza maeneo ya umwagiliaji. Utoaji wa mafunzo unalenga kuboresha ubora wa skimu na uendelezaji wa maeneo ya umwagiliaji unalenga kupanua maeneo ya umwagiliaji, kwa ujumla lengo kuu ni kuwa maendeleo endelevu ya umwagiliaji.

Muonekano wa kuendeleza umwagiliaji kwa hatua			
	Muda mfupi (2003 -2007)	Muda wa kati (hadi 2012)	Muda mrefu (hadi 2017)
<b>Lengo la maendeleo</b>	Kuazisha mfumo wa maendeleo endelevu wa umwagiliaji ifikapo 2017		
<b>Swala kuu kwa muhula</b>	Matengenezo	Madaraka Mikoani	Kujitegemea
<b>Uboreshaji masomo</b>			
<b>Njia za mkakati</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Kuendeleza mazingira kwa kukuza madaraka Mikoani na sekta binafsi</li> <li>- Kuanzisha teknolojia sahihi ya umwagiliaji wenye gharama nafuu</li> <li>-Kueza dhana ya mfumo wa kuendeleza mabonde ya mito</li> <li>-Kuanzisha mfumo wa kuendeleza umwagiliaji kwa mfumo shirikishi</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>-Kuendeleza umwagiliaji halisi kwa mbinu za serikali za mitaa chini ya madaraka mikoani</li> <li>- Kutumia teknolojia sahihi kuendeleza umwagiliaji wenye gharama nafuu</li> <li>- Kuanzisha hifadhi ya mazingira juu ya umwagiliaji</li> <li>-Kuanzisha mfumo wa umwagiliaji unaoendeshwa na wakulima</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Uanzishaji wa ufikaji kirahisi wa wakulima katika misaada ya kiufundi</li> <li>- Kueza njia za kuhifadhi mazingira zilizoanzishwa</li> <li>- Kuanzisha maendeleo ya umwagiliaji yenye kujitegemea kwa watu binafsi na serikali</li> </ul>
<b>Shughuli</b>	Andaa na tumia njia za programu za uboreshaji kwa miradi endelevu		
<b>Kuendeleza mradi</b>			
<b>Njia ya mkakati</b>	Panua eneo la kumwagilia kwa kuendeleza miradi ya umwagiliaji kwa kutumia ras ilimali za Taifa		
<b>Shughuli</b>	Toa kipaumele kwa kukarabati miradi midogo ya umwagiliaji na miradi ya uvunaji maji		
<b>Tarajio la ukuaji wa GDP kwa mwaka</b>	5.8 % to 6.0 %		

**【Programu ya Kuboresha Utoaji wa Mafunzo】**

Programu hii ina vipengele vingi nazo ni: (i) Taasisi (ii) Oganizesheni (iii) Masuala ya kiufundi (iv) Takwimu na udhibit wa taarifa (v) Mazingira. Programu thelathini na saba zilisaniifiwa kutokana na matokeo ya warsha ya PCM, uchambuzi wa matatizo pmoja na upimaji wa kuhakiki.

**【Programu ya kuendeleza maeneo ya umwagiliaji】**

Skimu za umwagiliaji 1,428 zenye ukubwa unaokadiriwa kuwa hekta 854,000, lilipangwa kwa kipaumbele kwa kufuata vigezo sita na kuwekwa katika makundi matano.

**Vigezo kwa kipaumbele cha mradi**

Kigezo cha ufundi	Kigezo cha uchumi	Kigezo cha mazingira	Urahisi wa kutekelezeka	Kigezo cha kijamii	Hali ya Mkoa	Jumla
Alama 15	Alama 30	Alama 10	Alama 5	Alama 20	Alama 20	Alama 100

Kufuatana na kipaumbele cha skimu za umwagiliaji pamoja na bajeti ya maendeleo, uendelezaji wa maeneo ya umwagiliaji umekadiriwa kama ifuatavyo:




**Maeneo ya umwagiliaji yatakayoendelezwa**

Maelezo	Muda mfupi	Muda wa kati	Muda mrefu
	2003 - 2007	Hadi Kufikia 2012	Hadi kufika 2017
(a) Idadi ya skimu	141	305	626
(b) Maeneo ya umwagiliaji yatakayo endelezwa	265,200 ha	324,900 ha	405,400 ha

**【Programu za maendeleo ya mkoa】**

Eneo Eneo lipatalo hekta 405,000 litachangia katika kufanikisha azma ya taifa katika kujitosheleza katika uzalishaji wa mpunga ifikapo mwaka 2017. Kwa kuongeza, viwango vya uzalishaji wa mpunga katika ngazi ya mkoa viliangaliwa kwa kutilia maanani sera ya “Zao zuri katika ardhi nzuri”. Matarajio ya mahitaji ya mpunga yalilinganishwa na uendelezaji wa skimu zilizopewa kipaumbele, matokeo yake yalibainisha kuwa, uzalishaji wa mpunga wa ziada ifikapo 2017 utatokea katika mikoa saba ambayo ni Pwani, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Rukwa na Ruvuma.



**Ufunguo**  
 150% ≤ SSR  
 100% ≤ SSR < 150%  
 50% ≤ SSR < 100%  
 SSR < 50%  
 Maji  
 Kielelezo: SSR – Ni uwiano wa uzalishaji na mahitaji ya mchele.

Kwa kuangalia tofauti ya uzalishaji na hali ya barabara, ramani ya mpango wa ugawaji iliandaliwa kama inavyoonyeshwa hapo kulia.

**【Hitimisho】**

Upembuzi unatoa mfumo na seti za mikakati kwa ajili ya umwagiliaji endelevu kwa Tanzania bara ifikapo mwaka 2017, kusudi kubwa ni kuchangia katika kuandaa mazingira mazuri yatakayoweza kuboresha uzalishaji na faida katika sekta ya kilimo. Ili kufikia lengo hili, upembuzi uliandaa programu ya maendeleo ya kuelekea mwaka 2017, katika suala hili, vipengele thelethini na saba vya programu ya kuboresha mafunzo vimeandaliwa na miradi pamoja na skimu 626 za kuendelezwa kwa utaratibu wa kupanua maeneo ya umwagiliaji.

Katika kuandaa programu ya maendeleo, upembuzi ulianzisha mfumo wa kutoa kipaumbele katika kuandaa skimu kwa ajili ya kuendelezwa na kutumia takwimu na taarifa zilizopatikana katika zoezi la kuhakiki. Upatikanaji wa takwimu na taarifa muhimu za skimu huathiri kwa kiasi kikubwa utoaji wa kipaumbele hivyo ni muhimu kupitia upya kipaumbele mara takwimu mpya zinapopatikana.

Upembuzi unahitimisha kuwa, utekelezaji wa programu hizi pamoja na kushirikisha vizuri sekta nyingine, taifa litakuwua na uwezo mkubwa katika kufikia ma hitaji ya mpunga ifikapo mwaka 2017.

**Kiambatanisho-3**

*Maelezo ya Ziada juu  
ya Uchambuzi Kiuchumi wa Skimu*

## Maelezo ya Ziada juu ya Uchambuzi Kiuchumi wa Skimu


Kabla ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo, uchumi, jamii husika, ufundi, mazingira na uhai wa mradi ungehakikishwa.

Uhai wa mradi kiuchumi utahakikiwa kwa kutumia njia zifuatazo:

(1) Kutambua eneo la maendeleo


Hali halisi 1 (Hali halisi ya Mpango wa Fursa na Vikwazo uliopendekezwa na kijiji)

Eneo linalopendekezwa kumwagiliwa maji na wanakijiji.




Hali halisi 2 (Hali halisi baada ya kufikia makubaliano juu ya eneo lililo pendekezwa)

Eneo inalofaa linaweza kuwa kubwa kuendeleza kutokana na ufinyu wa bajeti.




### Hali halisi 3 (Hali halisi baada ya uchunguzi wa uwiano wa maji)

Eneo lote lililopendekezwa linaweza lisimwagiliwe kutokana na uhaba wa maji.



### Hali halisi 4 (Uamuzi wa kuendeleza eneo)

Katika mfano huu, eneo linalomwagilia wakati wa mvua limechukuliwa kama eneo la kuendeleza, kuwa ni dogo kuliko eneo lililopendekezwa.





### Tahadhari

Mara baada ya kuamua eneo la kuendeleza, eneo hilo ndilo litakalotumika kufanyaiwa uchambuzi kiuchumi, usirejee eneo lote linalofaa au lililopendekezwa. Kwani hali katika eneo linalo endelezwa haibadiliki kwa kuendeleza umwagiliaji, lingeweza kuachwa baada ya uchambuzi wa kiuchumi.

(2) Tathimini ya kiuchumi

Hali ya kutokuwepo mradi


Hali ya kutokuwepo mradi inamaanisha kwamba, hali halisi ya eneo linalokusudiwa kuendelezwa lilivyo kwa wakati huu.



Linganisha hali ilivyo katika eneo lilelile (Eneo litakalo endelezwa) na lile lisilo lisilo

Hali ya kuwepo mradi

Hali ya kuwepo mradi inamaanisha kwamba, hali halisi ya eneo la kuendelezwa baada ya kuendelezwa.



Ongezeko la manufaa ya kilimo = b) - a)

Kabla ya kuanza uendelezaji ni muhimu kuthibitisha kwamba gharama za mradi (uwekezaji) si kubwa kuliko ongezeko la manufaa yatoakanayo na kilimo (matokeo baada ya uwekezaji). Hata hivyo ulinganifu kati yao hautoshi, kwa sababu ya kupungua thamani ya fedha ndani ya uhai wa mradi (yaani miaka 30) ungefikiriwa. Uchambuzi wa IRR (Internal Rate of Return) yaani kiwango cha faida ya ndani, inaweza kutoa jibu la uwekezaji dhidi ya ulinganifu wa faida kwa kuzingatia kupungua thamani ya fedha.